SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Wanafunzi** wote waliofaulu la 7 kuingia sekondari

UKURASA 4



**XAVI KUMBAKIZA DE JONG**

UKURASA 22

Nipashe
Jumanne Januari 4, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0579815
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

# NDUGAI: NIMEKOSA MIMI

●●● **Amwomba** msamaha Rais, Watanzania kutokana na kauli yake...

*Endelea ukurasa 2*



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake bungeni jijini Dodoma. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa kampeni ya kuhamasisha Watanzania kutumia huduma na bidhaa bunifu za benki hiyo, kufanikisha malengo yao kwa mwaka 2022, iliyoitwa 'Unachostahili ni CRDB Bank', jijini Dar es Salaam, jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Scania ilivyoua 14 kwenye unyago, vifo vitatu vyazua taharuki

UKURASA 2 & 3

**MICHEZO** **LEMA KUISUKA TENA YANGA PRINCESS** UK.23 **MAONI, KATUNI** UK.6



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake bungeni jijini Dodoma, kuhusu taarifa zilizoenea kwenye mitandao, aliomba radhi kwa kunukuliwa vibaya kuhusu Rais Samia Suluhu Hassan. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Ndugai: Nimekosa mimi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SPIKA wa Bunge, Job Ndugai, amemwomba radhi Rais Samia Suluhu Hassan na Watanzania kwa kauli yake iliyosambazwa katika mitandao ya kijamii ikimwonyesha kupinga mikopo inayokopwa na serikali ya awamu ya sita.

Ndugai, aliomba radhi jana jijini Dodoma alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kipande cha video yake iliyosambazwa kwenye mitandao ya kijamii na kuzua mijadala mkubwa kwenye mitandao ya kijamii na wadau mbalimbali wakiwamo wanasiasa, mwishoni mwa mwaka jana.

"Wakati tunaingia mwaka mpya mwezenu nilipata homa kali na hali ilikuwa ni mbaya sana, lakini katika kipindi hicho ndipo kulizuka mambo kwenye mitandao ya kijamii na mimi sikuwa na uwezo wa kuzungumza jambo lolote kuhusu 'clip' hiyo.

"Lakini leo nimeona niwaite ili niweze kutoa ufafanuzi kuhusu jambo hilo, Desemba 26, mwaka jana nilialikwa na kikundi kimoja cha Wagogo, lakini katika sehemu ya mazungumzo yangu niliongelea sana umuhimu wa kulipa kodi, ushuru na tozo mbalimbali nikihimiza tujitegemee na sio kama ambavyo watu walivyo kata sehemu ya hotuba yangu na kuiweka kwenye mitandao ya kijamii," alisema Ndugai.

Akirejea mazungumzo yake katika mkutano huo, alisema alisisitiza suala la ulipaji wa kodi pamoja na tozo huku akitoa msisitizo wa tozo ya miamala ya simu iliyopitishwa na bunge lake.

"Mimi haiwezi kutokea na wala haitatokea kupinga mikopo ambayo imekopwa na Rais wetu Samia Suluhu Hassan ambayo imeiwezesha nchi kufanya mambo makubwa sana katika ujenzi wa madarasa nchi nzima," alisema.

Katika wilaya yake alisema wamepewa madarasa 180 ambayo yote yanajengwa kwa fedha hizo na kuondoa kero iliyokuwa ikiwakabili kwa muda wote ya upungufu wa vyumba vya madarasa.

"Nitakuwa mtu wa kubeba dhambi kama nitapinga mikopo inayokopwa na Rais kwani mimi madarasa yote nimeyatembelea na nimeona ambavyo fedha hizi zimesaidia kupata madarasa mazuri sana na yenye viwango kama ilivyo ofisi hii hapa.

"Na wabunge wanakuja kwenye kikao cha bunge mwezi ujao mtawasikia wote ambao watatoa ushuhuda kuhusu mambo mazuri yaliyofanyika kupitia fedha hizi za mkopo wa trilioni 1.3, hawa wanaotaka kutuchonganisha na rais washindwe na walegee," alisema.

Akizungumzia mkopo uliokopwa na Rais, alisema umewezesha nchi kupeleka kiasi kikubwa cha fedha kwenye miradi ya maendeleo kuliko kipindi kingine chote.

Pia alisema mikopo imewezesha utekelezaji wa bajeti ya serikali kuwa rahisi kuliko kipindi cha nyuma ambacho fedha zilikuwa hazipelekwi kama zilivyo pangwa.

"Wakati wa nyuma ilikuwa ni vurugu unakuta mnapanga bajeti kwenda eneo fulani, lakini ukija mwisho wa mwaka unakuta fedha zimehamishwa kwenda katika kitu kingine na zingine zinapelekwa kiasi kidogo.

"Lakini kama kuna sehemu nilihisiwa kuwa kuna jambo nimezungumza la kumvunja moyo Rais wetu naomba radhi sana, anisamehe nimekosa mimi, nimekosa mimi, nimekosa sana, Mungu anisamehe, Watanzania wanisamehe," alisisitiza Ndugai.

Alifafanua kuwa katika kauli yake hiyo alikuwa na lengo la kuonyesha vile ambavyo walipitisha tozo ya miamala ya simu ambayo ililalamikiwa na watu ndiyo maana alisema watu watapima kama wataendelea nao mwaka 2025 au wataleta watu wengine.

"Miaka ya 1980 wengi hapa mlikuwa bado hamjazaliwa bunge lilipitisha sheria ya kulipa kodi ya kila kichwa cha mfugo na matokeo yake katika uchaguzi uliofuata wabunge wa mikoa yote ya wafugaji hawakurudi, lakini bunge liliwahi kufuta APEX na baada ya chombo hichi kufutwa wabunge wa mikoa inayolima tumbaku hawakurudi wakiwamo Said Nkumba na kina Vita Kawawa, waliobahatika ni kina Kigwangwala," alisema Ndugai.

Ndugai alisema amewasamehe wote ambao kwa kipindi hiki wamemtukana matusi kwa kuwa hawajui walitendalo.

"Waliotoa matusi tuwasamehe bure hawalijui walitendalo wengine pia bado wadogo," alisema.

Akisisitiza kauli yake, Spika Ndugai, alisema Bunge limeandaa siku ya kuliombea taifa ambayo itafanyika Januari 29, 2022 na Rais Samia anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Aliwakumbusha wabunge kujiweka tayari na vikao vya bunge mwezi ujao huku akizitaka kamati za bunge kufika Dodoma kuanzia Januari 16 na ya Ukimwi Januari 9.

# Scania ilivyoua 14 kwenye unyago

**Na Abdallah Khamis,** NEWALA

WATU 14 wamefariki dunia na wengine 22 kujeruhiwa baada ya gari aina ya Scania Boza lenye namba za usajili T 622 AFS, linalotumika kubeba maji kuwagonga waliokuwa kwenye sherehe ya unyago katika kijiji cha Lindumbe, Wilaya ya Newala Mkoa wa Mtwara.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Marc Njera, alisema kuwa juzi majira kati ya saa 2:00 na 2:30 usiku katika kijiji hicho gari hiyo iliyokuwa katika mwendo wa kasi liliwagonga watembea kwa miguu, waliokuwa wakitoka katika sherehe hizo.

Alisema baada ya ajali hiyo dereva alikimbia na kwenda kuliacha gari katika moja ya vituo vya mafuta kijijini hapo, huku jitihada za kumtafuta zikiendelea.

"Gari hili lilikuwa linatokea Newala kwenda Mahuta likiwa katika mwendo kasi, dereva wake alishindwa kulidhibiti na kwenda kuwagonga wananchi waliokuwa wakitumia barabara hii na kusababisha vifo na majeraha haya kwa ndugu zetu," alibainisha Njera.

Akizungumza katika eneo la ajali, Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, alisema ajali hiyo ni pigo kwa nchi kwa kuwa imepoteza nguvu kazi huku wengine wakibaki na majeraha makubwa.

Alisema ni muhimu kwa madereva na wananchi kuzingatia matumizi sahihi ya barabara wakati wote wanapotumia barabara.

"Tunaposikitika kwa ajili ya ajali hii sisi tulio hapa tuna jambo la kujifunza juu ya matumizi sahihi ya barabara tunawapa pole sana waliohusika katika ajali hii, lakini ni muhimu kuzingatia hatusababishi matukio kama haya kujitokeza tena.

Aliongeza kuwa serikali itashirikiana na ndugu wa marehemu kuwahifadhi wale wote waliopoteza maisha katika ajali hiyo, pamoja na kuhakikisha waliopata majeraha mbalimbali wanatibiwa na kurudi katika hali zao za kawaida.

MASHUHUDA

Mmoja wa mashuhuda wa ajali hiyo, Said Mwendo, alisema akiwa pembezoni mwa barabara muda huo wa usiku waliona gari lililowagonga wenzao likiwa katika mwendo wa kasi na ghafla wakasikia sauti ya baadhi yao wakipiga kelele za kuomba msaada.

Alisema gari hilo halikupiga honi wala kuwasha taa hali iliyowafanya wananchi waliokuwa wakitembea barabarani walisikie wala kuliona ili kuchukua tahadhari.

Naye Mariam Jumbe, alisema waliokuwa barabarani hawakuweza kusikia mngurumo wa gari kwa kuwa walikuwa wakifuatisha midundo ya ngoma kutokana na sherehe za unyago zilizokuwa zikiendelea eneo hilo.

MAJERUHI WAFUNGUKA

Fadhila Yusuf, aliyeumia mguu alisema kabla ya ajali alikuwa na wenzake wakitokea kucheza ngoma na kuingia barabarani wakiwa katika kikundi, waliona gari likiwa mbali huku likiwa limewasha mwanga mdogo mithili ya tochi kisha mwanga huo ukazimwa na ghafla gari likaongeza mwendo na kuwavamia waliokuwa katikati ya barabara wakicheza ngoma.

"Wengi wamekufa, wengine wameumia miguuni na vichwani mimi nilibahatika nikarushwa pembeni na kupata michubuko miguuni inauma sana rafiki zangu wamepoteza maisha," alisema Fadhila.

Majeruhi mwingine Swamadu Hassan, aliyeumia miguu, alisema alijikuta yupo katikati ya uvungu wa gari, lakini hakumbuki kama gari lilikuwa na taa au lilipiga honi.

Shamte Bakari aliyejeruhiwa kichwani katika ajali hiyo, alisema walikuwa wakicheza muziki wa singeli na ghafla wakasikia honi na kisha wakajikuta wamerushwa pembeni ya barabara wakiwa wamejeruhiwa.

"Tulikuwa tunacheza muziki wa singeli na honi ilipigwa gari likiwa limeshatufikia na wengi hatukusikia kutokana na kelele za muziki ndiyo tukajikuta tayari tumeshajeruhiwa na wenzetu kupoteza maisha," alisema Shamte.

Kaimu Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Newala, Mohamed Halifa Mohamed, alithibitisha kupokea miili ya marehemu 13 na majeruhi 23 na wakati wakiendelea na matibabu majeruhi mmoja alifariki dunia na kufanya idadi ya waliofariki kuwa 14 na majeruhi kubaki 22.

Alisema baada ya huduma za awali majeruhi wanane walihamishiwa Hospitali ya Ndanda, mkoani Mtwara kwa huduma zaidi huku wengine 14 wakiendelea na matibabu hospitalini hapo.

Alisema kati ya majeruhi hao, 14 waliobaki Newala wakiwa na majeraha madogo wanaume wanane na wanawake sita miongoni mwao mmoja ni mtoto.

HABARI KITAIFA

## Waganga tiba asili wahamasisha chanjo UVIKO-19

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAGANGA wa tiba asili na tiba mbadala wilayani Kahama, mkoani Shinyanga, wamejitosa kutoa elimu kwa jamii ya namna ya kujikinga na UVIKO-19 na umuhimu wa chanjo.

Mratibu wa shirikisho tiba asili Kanda ya Magharibi mikoa ya Tabora, Shinyanga na Kigoma, Athumani Waziri, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na gazeti hili ofisini kwake wanavyoshiriki kutoa elimu ya chanjo ya UVIKO-19.

Alisema waganga wa tiba asili na tiba mbadala wamekuwa wakipokea wagonjwa wengi kutoka sehemu mbalimbali, lakini wengi hawachukui tahadhari ya ugonjwa huo na hawajachanja.

"Hivi karibuni tulipata mafunzo maalumu ya UVIKO-19 jijini Dodoma na tukaagizwa kutoa elimu ya ugonjwa huu kwa wateja wetu juu ya muhimu wa chanjo na kuhakikisha wanavaa barakoa, kunawa mikono na maji tirirka na kukaa umbali wa mita moja wakati tukiendelea kutoa matibabu," alisema Waziri.

"Tumeanza kutoa elimu hii kwa waganga wa jadi wa Halmashauri ya Ushetu na baadaye tunaelekea kwa waganga wa jadi mkoani Kigoma, lengo letu ni kuhakikisha waganga wetu wanafanyakazi katika mazingira salama, wasipate ugonjwa huu ambao ni hatari kwa afya zetu na wateja."

Kadhalika, Waziri alisema halmashauri hiyo ina zaidi ya waganga wa tiba 230 kati ya hao 120 wamesajiliwa na wanatambulika kisheria na serikali na kwamba atakayekwenda kinyume na maelekezo ya Wizara ya Afya atawajibika kisheria.

Waziri alisema awali waganga wengi walishindwa kujitokeza kupata chanjo ya UVIKO-19 kwa kuhofia watageuka kuwa nyati baada ya uwapo wa uvumia mitandaoni na vijiweni kuwa chanjo hiyo sio salama, lakini baada ya viongozi wa kiserikali ikiwamo Rais Samia Suluhu Hassan kupata chanjo wamejitokeza kwa wingi.

Naye Colletha Kapongwa alisema kuwa utoaji wa elimu ya umuhimu wa chanjo kwa wateja wanaofika kwa waganga wa jadi kupata matibabu itasaidia kuondoa dhana ya kurogwa hasa kwa wananchi wanaoishi pembezoni mwa miji ambayo kila tatizo linalowatokea wanaamini ni imani za kishirikina.

Vile vile, alisema elimu ya ugonjwa huo kwa wananchi wanaoishi vijijini haikufika kwa haraka ikilinganishwa na wanaoishi mijini, baada ya wengi kukimbilia kwa waganga wa jadi.

Kwa upande wake, Mratibu wa chanjo ya UVIKO-19 Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, Mkola Vedasto, alisema wamepokea jumla ya dozi 24,142 na zilizotumika 18,079 sawa na wananchi 15,541 waliokwisha pata chanjo ya ugonjwa huo.

Alisema, awamu ya kwanza walipokea dozi ya chanjo ya J&J dozi 3,000, awamu ya pili 2,000 na tatu 455 na zote zilikwisha Novemba, mwaka jana na sasa wanaendelea na Sinovac 16,923 pamoja na dozi ya Pfizer 1764 na mwitikio wa wananchi ni mdogo na kuchanja mpaka wafuatwe.

# Vifo 3 vya ghafla viongozi h'shauri vyazua taharuki

**Na Samson Chacha ,** TARIME

WAKUU wa Idara watatu katika Halmashauri za Tarime Mjini na Tarime Vijijini, mkoani Mara, wamefariki kwa kipindi cha wiki moja na kuzua taharuki.

Waliofariki ni Ofisa Mipango Halmashauri ya Tarime Vijijini, Fredrick Mallya, Ofisa Elimu Taaluma Sekondari, Godfrey Mafumya (Tarime Vijijini) na aliyekuwa Ofisa Mifugo Halmashauri ya Mji wa Tarime, Pedas Masungwa.

Wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime Mji, Daniel Komote na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Tarime Vijijini, Saimon Kles, walithibitisha kutokea kwa vifo hivyo ndani ya wiki ya sikukuu ya Krismasi na Mwaka Mpya.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Tarime Vijijini, Solomon Shati na Tarime Mji, Gimbana Ntovya, walisema; "Halmashauri zetu hizi mbili katika kuufunga mwaka tumewapoteza watumishi wetu watatu ambao walikuwa wakuu wa idara na kwamba ni pigo kubwa, lakini wanamshukuru Mungu.

Walisema Ofisa Mipango Halmashauri ya Tarime Vijijini, Mallya, aliugua ghafla Januari mosi, mwaka huu na kukimbizwa Hospitali ya Rufani Bugando Mwanza na umauti kumkuta huko.

Shati alisema Ofisa Elimu Taaluma Sekondari, Mfumya, aliugua mwishoni mwa Desemba, mwaka jana na kukimbizwa Hospitali ya Bugando na kufariki dunia.

Kwa mujibu wa Ntovya, aliyekuwa Ofisa Mifugo Halmashauri ya Mji Tarime, Pedas Masungwa aliyefariki usiku wa Desemba 26, aliugua ghafla akiwa nyumbani alikutwa na mauti wakati akikimbizwa hospitalini.




Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba (katikati), akizungumza katika kipindi cha Jambo kuhusu msamaha wa tozo kwa waajiri wenye malimbikizo ya michango. PICHA: MPIGAPICHA WETU

## NSSF yakusanya bil. 17/- kampeni msamaha wa tozo

**Na Mwandishi Wetu**

MKURUGENZI Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, amesema kampeni ya msamaha wa tozo inayolenga kuwahamasisha waajiri wote wa sekta binafsi kulipa michango yao imepata mwitikio mkubwa na katika kipindi cha miezi mitatu wamekusanya wastani wa Sh. bilioni 17 kupitia kampeni hiyo.

Mshomba alisema hayo jana katika kipindi cha Jambo cha Televisheni ya Taifa ikiwa ni sehemu ya kampeni ya mwezi ya kuwahamasisha waajiri kulipa malimbikizo ya michango yao ili waweze kunufaika na msamaha wa tozo kwa asilimia 50 kwa watakaolipa kuanzia Januari 1 hadi 31, 2022.

Alisema kampeni hiyo ilianza mwezi Oktoba, 2021 na inahusu waajiri wote wa sekta binafsi wenye malimbikizo ya michango kwa kipindi kilichoishia Juni 30, 2021.

Mshomba alisema katika kipindi hicho, waajiri wote waliolipa malimbikizo ya michango yao kuanzia Oktoba 1, 2021 mpaka Novemba 30, 2021 walinufaika na masamaha wa tozo kwa kiwango cha asilimia 100.

Alisema kwa waajiri waliolipa malimbikizo ya michango kuanzia Desemba 1 hadi 31, 2021 walipatiwa msahama wa tozo kwa kiwango cha asilimia 75.

"Kwa sasa Mfuko wa NSSF unaendelea na kampeni kabambe ambayo ni mwendelezo wa kuhamasisha waajiri kulipa michango yao ili waweze kunufaika na msamaha wa tozo kwa asilimia 50," alisema Mshomba.

Alisema tozo zinasababishwa na mwajiri mwenyewe kutolipa michango kwa wakati kwa sababu kwa mujibu wa Sheria ya NSSF waajiri wote katika sekta binafsi wanapaswa kulipa michango asilimia 20, ambapo asilimia 10 atakata kutoka katika mshahara wa mfanyakazi wa kila mwezi na asilimia 10 mwajiri, lakini mwajiri anaweza kulipa kubwa zaidi.

Alisema lengo la NSSF kuja na msamaha huo ni kuwaondolea mzigo waajiri kwa kuwa tozo hizo ni kubwa na mzigo kwa mwajiri huku akisisitiza kuwa, msamaha huo pia unalenga kuboresha mazingira ya biashara zao kwa kuwa fedha ambayo walipaswa kulipa kama tozo wataitumia katika shughuli zingine za maendeleo ya taasisi zao.

Mshomba alifafanua kuwa, tozo zinasababishwa na waajiri wenyewe kwa kutolipa michango kwa wakati kama sheria inavyosema, alitoa wito kwa waajiri kuchangamkia fursa hiyo ndani ya mwezi huu wa Januari ili waweze kupata msamaha kwa asilimia 50.

Alibainisha kuwa, NSSF imeweka kipaumbele katika kuelimisha waajiri wa sekta binafsi na umma kwa ujumla kuhusiana na msamaha huo pamoja na umuhimu wake ili waweze kuelewe vizuri.

Mshomba aliwasisitiza waajiri kwenye sekta binafsi nchini kuwasilisha michango yao kwa mujibu wa sheria na kuepuka kukumbana na tozo.



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, akiwa na wataalamu wa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS), Mkoa wa Dar es Salaam alipokagua maendeleo ya ujenzi wa barabara ya Morogoro, Kimara – Kibaha (njia nane), jana. PICHA: MPIGAPICHA WETU

# Wanafunzi wote waliofaulu la 7 kuingia sekondari

**Na Salome Kitomari**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amesema wanafunzi 9,780 waliofaulu darasa la saba mwaka jana, wataingia kidato cha kwanza Januari 17, mwaka huu, baada ya vyumba vya madarasa 15,000 kukamilika ujenzi.

Akizungumza jana wakati wa uzinduzi wa Bodi ya Wakurugenzi wa Huduma za Maktaba Tanzania (BOHUMATA), alisema nguvu kubwa ya serikali ni kuboresha elimu ili wanafunzi wasome vizuri, na wajibu wa watendaji ni kusimamia na kuchapa kazi ili malengo yaliyowekwa yafikiwe kwa ufanisi.

Alisema madarasa hayo yamejengwa kwa fedha za UVIKO-19 na sasa nchi ina uhakika wanafunzi wote waliofaulu wataendelea na masomo yao na hakuna atakayekaa nyumbani.

Alisema ndani ya miezi tisa wizara hiyo imepata fedha za kuendeleza elimu ya juu, Dola za Kimarekani milioni 425 sawa na Sh. milioni 982, na kwamba mradi mwingine ni kuimarisha elimu ya sekondari utakaogharimu Dola za Marekani milioni 500 sawa na Sh. trilioni 1.15 ambazo zimepelekwa kwenye halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari 245.

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, katika kila eneo zimetengwa Sh. milioni 600 kwa ajili ya kujenga shule mpya na kwamba hadi mwaka 2025 zitajengwa shule za sekondari za wasichana 26 na kwa kuanzia wameanza ujenzi kwenye mikoa 10 na fedha zimeshapelekwa.

"Nitakuwa mkali kweli kweli, sitakubali mtu achezee hata senti tano ya fedha ambazo zimeletwa kwa ajili ya kuboresha sekta ya elimu, naiomba Bodi isimamie kikamilifu, waulize sana wakati mwingine watendaji wanaona kama bodi inapitiliza, lakini watambue ndiyo yenye dhamana itapitiliza vipi, naomba simamieni vizuri mtu asiwatie woga kwa namna yoyote ile," alisema.

**MAKTABA MTANDAONI**

Prof. Ndalichako alisema ni muhimu bodi hiyo ikakamilisha uanzishaji wa maktaba mtandaoni ili kuwezesha Watanzania wengi kujisomea vitabu na machapisho kulingana na mahitaji ya rika zote.

Alisema bajeti imeongezeka Sh. milioni 424.2 hadi Sh. bil. 1.4 zilizowezesha kumudu gharama za uwekezaji kuanzia ofisi za tarafa hadi taifa, huku ikiongezeka kutoka Sh. milioni 500 mwaka 2020/21 hadi Sh. bilioni 10.5 mwaka 2021/22, na kwamba lazima zisimamiwe kufikia malengo husika.

"Shilingi bilioni mbili zitatengeneza maktaba mtandao, bilioni tatu, ukarabati wa jengo la Maktaba Kuu ya Taifa, shilingi bilioni 3.5 za ujenzi wa maktaba Wilaya ya Chato na shilingi bilioni 1.5 ni za ununuzi wa samani katika vituo 43 vya maktaba na shilingi milioni 500 kwa ajili ya jengo la maktaba ya Arusha," alifafanua.

Kwa mujibu wa Prof. Ndalichako, ni muhimu kuwa na vitabu vya kuwawezesha wananchi kujenga uwezo kwenye shughuli zao za kila siku, kwa kuhakikisha wanataaluma, wakulima au wajasiriamali wanapata vitabu na machapisho ya kuboresha shughuli zao kwa kuwa lengo la nchi ni kuendeleza utamaduni wa kujisomea kwa kutumia maktaba zitakazojibu kiu yao.

Aidha, alisema majukumu ya bodi ya maktaba yameainishwa kwenye Sheria ya Bodi Namba 6 ya Mwaka 1975, na kwamba ni muhimu kumshauri kama inakidhi matarajio au kuna haja ya kuifanyia marekebisho ili iendane na mabadiliko ya sayansi na teknolojia nchini na duniani, huku akitolea mfano maktaba mtandao, sheria haijalizungumzia na kwamba ni muhimu kuangalia utoshelevu wake.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof. Rwekaza Mukandara, alisema watatekeleza majukumu yao kwa umakini na uadilifu katika kuboresha huduma za maktaba nchini, ambacho ni kisima cha ujuzi na maarifa, kwa kuwa kuna mkusanyiko wa maandiko ya masomo ya fani mbalimbali, ambayo yamemwongezea binadamu uelewa wa mazingira anamoishi na mbinu za kukabiliana na changamoto.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa BOHUMATA, Dk. Mtoni Ruzegea, alisema baadhi ya vipaumbele ni kwamba kila mwandishi au mchapishaji wa ndani ya nchi atawajibika kupeleka nakala mbili ya kazi zake kwa ajili ya kuhifadhiwa, kuwajengea uwezo na kuwaendeleza watumishi kimasomo.

# Shahidi adai Sabaya hakumheshimu mkuu wake

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa 13 katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabiri aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, upande wa Jamhuri, Ramadhani Juma (39), ameieleza mahakama kwamba Sabaya, hakuwa akimheshimu mkuu wake wa kazi ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Shahidi huyo ambaye ni Ofisa Uchunguzi kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), alitoa madai hayo jana kwa Hakimu wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Arusha, Patricia Kisinda.

Katika shauri hilo, mbali na Ole Sabaya washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), John Odemba, Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31).

Alidai mahakamani kwamba vijana wa Ole Sabaya walikuwa wakitekeleza jukumu la kuchukua fedha kwa Mroso kwa kuwa lilikuwa agizo kutoka kwake (Ole Sabaya).

Alidai kwamba baada ya kuondoka katika eneo la benki, katika uchunguzi wake alibaini Ole Sabaya pia alikuwa akiratibu genge la uhalifu.

Kadhalika alidai kubaini Jakson Macha na Mroso walitoka ndani ya benki (jina limehifadhiwa) wakiwa wamebeba fedha zikiwa zimewekwa kwenye boksi na kuingia kwenye gari la mfanyabiashara huyo na kuondoka.

Alidai kupitia picha za video zilionyesha vijana hao walikabidhiwa fedha hizo na mfanyabiashara, Francis Mroso wakiwa benki.

Pia alidai kupitia video hizo alibaini Jakson Macha alimzuia Mroso kuzungumza na simu wakiwa ndani ya benki.

Alidai alibaini walipotoka Wilaya ya Hai Januari 22, mwaka jana kwenda Arusha na kabla ya kufika kwa Mrosso, walifikia katika Hoteli ya Point Zone sehemu ambayo walipanga mipango yao kabla hawajaenda kwa mfanyabiashara huyo.

Shahidi huyo aliendelea kudai kuwa katika mbinu zao walikubaliana kumfunga pingu Mwahomange ili watakapofika kwa Mrosso ionekane amekamatwa na watu wenye mamlaka.

"Mbinu zao zilizaa matunda na Ole Sabaya alipofika kwa Mrosso alijitambulisha kwamba ni kikosi kazi maalumu kilichoteuliwa na aliyekuwa Rais Hayati John Magufuli, alikuwa ameongozana na maofisa wa Idara ya Usalama wa Taifa na TRA, kufuatilia na kuwabaini wakwepa kodi wote," alidai Juma.

Alidai kwamba mambo yote hayo aliyabaini kupitia taarifa za kiintelijensia na mahojiano ambayo tayari alikuwa ameshafanya na baadhi ya washtakiwa ambao ni Daniel Mbura na John Odemba.

Kadhalika alidai kuwapo na tukio la utakatishaji fedha kwa kuwa baada ya kupewa fedha hizo Ole Sabaya alikodisha chumba na kutoa mgawo wa fedha kwa vijana wake walioshiriki katika tukio hilo.

Alidai tukio la utakatishaji wa fedha alibaini kupitia taarifa fiche na maelezo aliyochukuwa kwa watuhumiwa akiwamo John Odemba na Nathan Msuya.

Vilevile, shahidi huyo alidai kwa mujibu wa mahojiano aliyofanya na Katibu Tawala Msaidizi wa Rasilimali Watu na Utawala mkoani Kilimanjaro, Sabaya hakuwa na kibali chochote cha kutoka katika kituo chake cha kazi.

Aidha, alidai kwamba Ole Sabaya akiwa Mkuu wa Wilaya ya Hai hakuwa na mamlaka halali ya kukusanya kodi na mamlaka yake yalikuwa ndani ya eneo lake la kazi.

Shahidi huyo alidai kwamba kwa kipindi cha Januari mwaka jana hakukuwa na kikosi kazi chochote kilichoundwa na Kamishna ya TRA kufuatilia masuala ya kodi katika Mkoa wa Arusha.

Katika hatuna nyingine, mahakama hiyo imeridhia pingamizi lililowekwa na mawakili wa upande wa utetezi wakipinga shahidi huyo kuzitolea ufafanuzi video za CCTV, wakidai kwamba si mtaalamu na hana uwezo wa kuzielezea.

# Njia nane Kimara-Kibaha kukamilika rasmi mwezi Juni

**Na Gwamaka Alipipi**

MRADI wa upanuzi wa barabara ya Morogoro (Kimara-Kibaha) njia nane awamu ya pili ikijumuisha ujenzi wa madaraja na barabara za kuingilia na kutoka unatarajia kukamilika Juni 21, mwaka huu.

Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam alipofanya ziara ya ukaguzi wa mradi huo.

Mhandisi Kasekenya alisema hadi sasa mradi huo awamu ya pili umefikia asilimia 12 na ulitengewa Sh. bilioni 57, kwamba unatekelezwa na mkandarasi mzawa aitwaye M/S Estim Construction Co. Ltd.

Akiwa katika ukaguzi wa barabara hiyo, Mhandisi Kasekenya alisema: "Barabara hii ilipaswa kukamilika Oktoba, mwaka jana, kwa gharama ya Sh. bilioni 161 kwa fedha za serikali.

"Lakini kutokana na mabadiliko na mahitaji baada ya ujenzi wa Kituo cha Mabasi cha Magufuli ikaonekana mahitaji ni makubwa, hivyo serikali ikatoka Sh. bilioni 57 ili kutengeneza madaraja na barabara za kuingia na kutoka."

Alibainisha kwamba awamu ya pili inajumuisha ujenzi wa madaraja mawili, la kwanza likijengwa katika eneo la kwa Yusuph na Mbezi Mwisho.

Mhandisi Kasekenya alisema ujenzi mwingine ni barabara za kuingia na kutoka katika Stendi ya Mabasi Magufuli, na barabara kutoka Mbezi ya zamani kutumiwa na mabasi ya mwendokasi.

Aidha, aliitaka menejimenti ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kuwasiliana na vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha mapipa yaliyowekwa katika mradi huo yanatumika vizuri.

Pia aliwataka wananchi kutumia alama za pundamilia na madaraja kuvuka katika barabara ya njia nane, huku akisisitiza kwamba madaraja hayo yamejengwa kwa ajili yao na siyo kupendezesha jiji.

Vilevile, aliwataka wananchi kutotupa taka ngumu katika mifereji akionya hali hiyo inasababisha mifereji kuziba nyakati za mvua.

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam, Harun Senguku, alisema mradi wa ujenzi wa barabara nane una urefu wa kilometa 19.2.

Alisema lengo kuu la serikali kujenga barabara hizo ni kufanya mtiririko wa magari yanayoingia na kutoka katika Jiji la Dar es Salaam kuwa rahisi, kupunguza gharama za usafirishaji.

"Mradi huu ulikuwa na awamu ya kwanza ambao ulimalizika ukiwa na gharama ya Sh. bilioni 161. Baada ya serikali ya awamu ya sita kuiingia madarakani tumeongezewa fedha zingine kwa ajili ya kupanua miundombinu ikiwamo ujenzi wa madaraja na njia za kuunga sehemu mbalimbali ikiwamo katika Kituo cha Mabasi Magufuli," alisema Senguku.

Alisema kwa sasa TANROADS Mkoa wa Dar es Salaam imeongezewa fedha ili kukamilisha sehemu ya kazi iliyobakia.

Naye Mhandisi Miradi TANROADS mkoa huo, Mwanaisha Rajabu, alisema changamoto walizokutana nazo mpaka sasa ni kuchelewa kuwasili kwa vifaa vya ujenzi kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa virusi vya corona.

"Mkandarasi aliagiza vifaa vya usalama barabarani kutoka Afrika Kusini, lakini vilichelewa kufika kutokana na mlipuko wa UVIKO-19 kulikosababisha baadhi ya viwanda kufungwa kwa muda."

## Ofisa mifugo akutwa amejinyonga

**Na Said Hamdani,** LINDI

OFISA Mifugo wa Kata ya Milola mkoani Lindi, Joel Nanjambwa (51), amekutwa amefariki dunia kwa kujinyonga kwa kile kinachodaiwa kuibiwa fedha kwa njia ya utapeli.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Mtatiro Kitinkwi, amethibitisha kutokea kwa tukio hilo lililotolea Desemba 28, mwaka jana na mwili wake kuonekana siku tatu baadaye.

Akifafanua kuhusu tukio hilo, Kamanda Kitinkwi alisema Desemba 28, mwaka jana, Nanjambwa aliondoka nyumbani kwake na hakurejea hadi Desemba 31, majira ya saa 11 alasiri mwili wake ulipokutwa katika pori la Kijiji cha Mkangaulani ukiwa unaning'inia juu ya mti.

"Mwili wa Nanjambwa umegunduliwa katika pori la Naiputa, Kijiji cha Mkangaulani akiwa amejinyonga kwa kutumia shati lake, ukiwa umeharibika," alisema.

Kamanda Kitinkwi alisema chanzo cha tukio hilo hakijafahamika na Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi ili kubaini sababu za kujinyonga kwa ofisa huyo wa serikali.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya ndugu na majirani wa karibu wa marehemu (majina yamehifadhiwa) walidai kwamba kujinyonga kwa Nanjambwa kumechangiwa na hasira ya kuibiwa fedha zake kwa njia ya utapeli.

"Huyu Nanjambwa alipata fedha zilizotokana na kubashiri, wajanja wakampigia simu na kuweleza walichomwambia na kukomba fedha zake zote," walidai mashuhuda hao.

Walidai kitendo hicho kilimchukiza mke wake na kuanza kumsemea maneno yasiyofaa, ndipo Nanjambwa akachukuwa uamuzi wa kujiua kwa kujinyonga.

Wakati huohuo, Kamanda Kitinkwi alipongeza utulivu uliooonyeshwa na wananchi katika kusherehekea kwa amani na utulivu sikukuu za mwisho wa mwaka, huku akitaka utaratibu huo uwe endelevu na kudumu katika Mkoa wa Lindi.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO
MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TMDA Tanzania Medicines & Medical Devices Authority

# TAARIFA KWA UMMA

**TAHADHARI YA UWEPO WA MATAPELI KWA WATEJA WA TMDA**

1. Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) inapenda kuutadharisha umma kuwa wamejitokeza matapeli ambao hujifanya kuwa ni watumishi wa TMDA. Watu hao hupiga simu au kutuma ujumbe mbali mbali kwa mfano ***"Habari – TMDA tunapenda kukujulisha huduma ipo tayari wasiliana nasi kwa namba hii ahsante";***
2. Matapeli hao hudai kuwa wanaweza kuwasaidia wateja kupata huduma zinazotolewa na TMDA kwa muda mfupi kuliko muda ulioainishwa katika ***Mkataba wa Huduma kwa Mteja.*** Baada ya kutoa taarifa hiyo, hutuma ujumbe mwingine au kupiga simu na kuomba kiasi fulani cha fedha ikiambatana na namba ya simu ambayo pesa hizo zinapaswa kutumwa;
3. TMDA inachukua fursa hii kuutahadharisha umma juu ya utapeli huo na kushauri kupuuza ujumbe wowote wa aina hiyo. Aidha, tunawakumbusha wateja kuwa huduma zetu hutolewa katika ofisi ya Makao Makuu Dodoma, ofisi ndogo ya Makao makuu Dar es Salaam, ofisi za kanda zilizopo Dar Es Salaam, Arusha, Dodoma, Geita, Mbeya, Mwanza, Mtwara na Tabora pamoja na vituo vya forodha na siyo kwa kificho kama ambavyo matapeli wanataka ieleweke;
4. Vile vile, huduma hizo hutolewa na mtumishi anayevaa kitambulisho na beji yenye jina la mtumishi husika ili iwe rahisi kwa mteja kumtambua pale inapohitajika;
5. Kwa tangazo hili, umma unakumbushwa kuendelea kupata huduma katika ofisi zetu zilizoko nchini kote na kuhakikisha kuwa malipo yote ya ada na tozo yanafanyika kupitia benki au mawakala waliothibitishwa na benki husika baada ya kupatiwa ankara kifani (Profoma invoice) na Namba ya Malipo ya Serikali (Control Number);
6. Aidha, tunawashauri wateja kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya matapeli hao na pale wanaposhawishiwa kupatiwa huduma nje ya ofisi za TMDA na kwa utaratibu tofauti, wasisite kutoa taarifa mara moja katika ofisi za TMDA nchini kote, kupiga simu bila malipo kupitia **Na. 0800110084** au kutoa taarifa kituo chochote cha Polisi kilicho karibu; na
7. TMDA inashirikiana na vyombo vya Ulinzi na Usalama kuwatafuta matapeli hao ili waweze kukamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Imetolewa na:

**Mkurugenzi Mkuu,**
**Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA),**
**S.L.P 1253, Dodoma Au**
**S.L.P 77150, Dar es Salaam**
**Simu: +255 22 2452108/2450512/2450751**
**Simu bila Malipo: 0800110084**
**Barua pepe: info@tmda.go.tz**
**Tovuti: www.tmda.go.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Elimu mbadala kwa wasichana iwe endelevu

**JUMLA** ya wasichana 3,000 wa umri kati ya miaka 13 hadi 21 waliokatiza masomo ya sekondari wanatarajia kuanza tena Januari 17, mwaka huu katika vituo mbalimbali nchini.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), Dk. Michael Ng'umbi, alisema wasichana watanufaika na masomo hayo kupitia Mpango wa Elimu Sekondari kwa njia mbadala chini ya mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari (SEQUIP- AEP).

Tayari serikali inatoa mafunzo kwa wadau wenye jukumu la kusimamia mradi huo katika uboreshaji wa miundombinu ya madarasa, kujifunzia na kufundishia kwenye mikoa 26 Tanzania Bara.

Alisema wasichana hao ni kati ya 12,000 watakaonufaika na mradi huo wa miaka mitano 2021-2026 wenye lengo la kuimarisha elimu ya sekondari nchini na TEWW imepewa jukumu hilo.

Hadi sasa tunaelezwa wasichana 1,500 kati ya 3,000 wamejiandikisha, ikiwa ni ufadhili wa Dola za Marekani milioni 500, na tunatarajia kuona thamani ya fedha ili hata zikiisha mradi uwe endelevu.

Hii ni habari njema kwa kuwa wasichana hawa ambao ndoto zao zilikaribia kuzimika kutokana na ujauzito au sababu nyingine zilizowafanya wasihudhurie darasani kwa mujibu wa sheria, na sasa kwa mpango huo tunadhihirisha kuwa elimu sio ya mfumo rasmi pekee bali hata njia mbadala inawezesha waliovuka umri wa kwenda shule kupata elimu.

Hii inakuja wakati ambako wasichana wengine waliopata mimba wanaruhusiwa kuendelea na masomo katika mfumo rasmi ndani ya miaka miwili tangu kuacha shule, maana yake fursa ya elimu kwa kundi hili ni kubwa kazi kwao sasa kuitumia.

Kupitia mpango huu sasa wataendelea na masomo na tutakuwa na madaktari, mawaziri, wakurugenzi, wakuu wa taasisi mbalimbali, walimu na kada nyinginezo zenye kuhitaji wataalamu.

Tunaipongeza serikali kwa kukamilisha mpango huu hasa kuhakikisha miundombinu muhimu ipo, walimu pamoja na vitabu vya kiada na ziada vitakavyowawezesha wasichana hawa kusoma kama wengine na kufikia malengo yao.

Tunaamini kama mfumo huu usingekuwapo wasichana hao wangeshindwa kufikia ndoto zao, lakini sasa wanakwenda kuendelea na masomo vinginevyo wangeishia kulea familia.


Hii ni fursa adimu inayopaswa kutumiwa kikamilifu na wasichana hao na haitarajiwi kuwapo kizuizi chochote kutoka kwa familia au kwasababu wana watoto basi waonekane jukumu lao ni kulea.

Kwa kuruhusu wasichana hawa kusoma sasa tunaendelea kuongeza idadi ya wanawake walisoma na kujitambua, lakini kwenye nafasi za maamuzi tutapata wanawake wengi ambao wamepitia changamoto na kujifunza umuhimu wa elimu.

Tunaamini kuwapo kwa mpango huu haitakuwa sababu ya wasichana wanaopata mimba kuongezeka, kwa kuwa wana uhakika wa kuendelea na masomo hata baada ya kujifungua bali iwe ni namna ya kujifunza kujirekebisha kwa kuwa elimu katika mfumo rasmi ni nzuri na inamfanya mwanafunzi kusoma kwa kuwa hana majukumu mengine. Ikiwa vituo hivyo vitatumiwa vyema itakuwa ni sehemu ya kupika wataalamu ambao watalisaidia taifa, na watatumika kutoa elimu kwa wasichana kutoa mifano yao wenyewe ya maisha yao, ili wengine wasipite njia waliyopita wao.

Haitarajiwi kuona vituo hivyo vinageuka kuwa magofu bali kisima cha elimu nzuri, ili baadaye itakapofanyika tathmini tuone manufaa ya kuwa na mpango huu unaruhusu waliokosa elimu kwenye mfumo rasmi kuipata kama ambavyo kulikuwa na Mpango wa Elimu kwa Waliokosa (MEMKWA), ambayo ilikuwa na vituo kwenye wilaya na mikoa nchini.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Vijana fursa hizo mkakati wa kukuza TEHAMA

**SERIKALI** imetangaza kuwekeza zaidi kwenye Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya mkongo wa taifa na kuusogeza hadi kila wilaya na kuondoa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwenye vifaa vya TEHAMA.

Katika dunia ya sasa, kumekuwapo na mabadiliko makubwa ya TEHAMA, ambayo inachukua nafasi kubwa ya kuharakisha maendeleo yakiwamo ya elimu.

Katika kufanikisha hilo, serikali inawekeza kwenye miundombinu ya mkongo wa taifa na kuusogeza hadi kila wilaya na kuondoa VAT kwenye vifaa vya TEHAMA, vifaa hivyo ni pamoja na vya kielektroniki simu janja na modemu, ili kuwajengea vijana mazingira bora ya kutumia teknolojia hiyo kujiajiri kwa ajili ya maendeleo yao na taifa.

Si hapo tu bali inasema, inatarajia pia kujenga chuo bora zaidi cha kisasa cha TEHAMA, ili kuongeza kasi, ubunifu na ufanisi katika matumizi ya teknolojia hiyo, kwa kuwa ndiyo ni msingi wa taifa endelevu.

Chuo kinachotarajiwa kujengwa na serikali kutatoa kipaumbele katika masuala ya utafiti na ubunifu kwenye TEHAMA, kwa kusajili na kuwatambua vijana wote wanaojishughulisha na teknolojia hiyo.

Ni wazi kwamba, serikali inataka kunyanyua ubunifu wa vijana, hivyo ni vyema vijana wenyewe wakachangamkia fursa hiyo, kwa kuonyesha uwezo wao wa teknolojia hiyo ambayo ina nafasi kubwa katika dunia ya leo.

Hiyo ni ahadi ya Rais Samia Suluhu Hassan kwamba, serikali yake itatoa kipaumbele katika kusaidia vijana watakaojiunga pamoja kwenye shughuli mbalimbali za utafiti na ubunifu kwenye TEHAMA.

Ni katika kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru mwishoni mwa mwaka jana wilayani Chato mkoani Geita anasema, dunia ipo kwenye mapinduzi ya nne ya viwanda, shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zinafanyika kwa TEHAMA.

**Ni wazi kwamba, serikali inataka kunyanyua ubunifu wa vijana, hivyo ni vyema vijana wenyewe wakachangamkia fursa hiyo, kwa kuonyesha uwezo wao wa teknolojia hiyo ambayo ina nafasi kubwa katika dunia ya leo.**

Kwamba, chuo hicho ambacho Rais anasema kitakuwa kinaongoza kwa ubora Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika, kitawajengea pia uwezo wa kimataifa, kujiingizia kipato na kwa maendeleo ya Taifa.

Uamuzi huo wa serikali unaonyesha ni jinsi gani imeamua kuweka nguvu kwenye teknolojia hiyo ili kwenda na wakati hasa katika karne ya 21 ambayo ni ya sayansi na teknolojia ili kuboresha huduma mbalimbali.

Ikumbukwe kuwa, dunia ya sasa, kumekuwapo na mabadiliko makubwa TEHAMA ambayo sasa inachukua nafasi kubwa kwa ajili ya kuharakisha shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo elimu.

TEHAMA imerahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali zikiwamo za elimu, lakinipia kupunguza upotevu wa muda na gharama za kusafiri kutoka eneo moja kwenda lingine kufuata mahitaji mbalimbali.

Kwa sasa, kila mtu anahitaji uelewa wa msingi wa teknolojia hiyo na jinsi inavyofanya mambo mbalimbali ikiwamo kuwa wanafunzi wazuri, kufundisha watu jinsi ya kuwa na uwezo wa kuitumia.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, katika karne ya 21, TEHAMA inahitajika katika stadi muhimu na mifumo ya elimu, lakini kwenye sekta mbalimbali kwa ajili ya kuharakisha maendeleo.

Katika viwanda na kwenye jamii ya kisasa kwa ujumla, inaelezwa kuwa teknolojia hiyo ina majukumu muhimu ya kimkakati kama njia mojawapo ya kuharahisisha shughuli za kila siku.

Hivyo, kutokana na umuhimu huo, Tanzania haijabaki nyuma, badala yake inachukua hatua kusonga mbele kwa kuwekeza katika teknolojia hiyo hasa kwa mkakati wa kujenga chuo kikubwa cha TEHAMA, lakini kutumia teknolojia hiyo kuendeleza vijana kupata ajira.

HABARI KITAIFA

# Rais Mwinyi aahidi makubwa kwa vijana

**Na Suleiman Omar,** PEMBA

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa Serikali ya Awamu ya Nane inalizingatia kundi la vijana kuwa ni maalumu lenye changamoto ambazo ni wajibu wa serikali kuzitafutia ufumbuzi.

Aliyasema hayo katika uzinduzi wa matembezi ya Jumuiya ya Vijana wa Chama Cha Mapinduzi wa mikoa yote ya Tanzania, katika kiwanja cha mpira Konde, Wilaya ya Micheweni, Mkoa wa Kaskazini Pemba ikiwa ni shamra shamra za maadhimisho ya sherehe za miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar Matukufu ya Januari 12, 1964.

Rais Dk. Mwinyi alisema, jitihada za serikali ni pamoja na kuimarisha ubora wa elimu inayotolewa katika ngazi mbalimbali pamoja na kuboresha mafunzo ya ufundi wa fani tofauti kwa vijana wanaojiunga kwenye vyuo vya mafunzo ya amali.

Alisema, hatua nyingine ni vijana kujiunga na mabaraza ya vijana yaliyoanzishwa katika wilaya zote za Unguja na Pemba ambayo shughuli zake zinasimamiwa na kuratibiwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

Vile vile, alisema uwapo wa mabaraza hayo ni jukwaa la kuwaunganisha vijana kubuni miradi ya kiuchumi na kuwapatia mitaji, taaluma na masoko ya kuuzia bidhaa zao. Ni matumaini yake kuwa mabaraza hayo yakiimarishwa vyema yatasaidia vijana kukabiliana na tatizo la ajira.

Alisema, ujenzi wa uchumi wa kisasa unaodhamiriwa kujengwa, una lengo la kuziendeleza jitihada za mafanikio ya awamu za uongozi uliotangulia, na kuelekeza nguvu ya kuleta mapinduzi ya kiuchumi.

Pia alisema licha ya changamoto zilizotokana na athari za UVIKO-19, Zanzibar imeanza kupiga hatua za kwenda ambako nchi imedhamiria, na kwamba wajibu wa wananchi wote kuunga mkono na kushirikiana na serikali katika kuyafikia malengo.

"Mimi binafsi nimevutiwa sana na utaratibu huu wa kuwajumuisha vijana kutoka maeneo mbalimbali ya nchi yetu na kuwa pamoja katika masuala haya ya kuhamasishana uzalendo na umoja pamoja na kukumbushana masuala muhimu ya mustakabali wa taifa letu," alisema.

Alisema kwa jitihada zao viongozi waliotangulia pamoja na wananchi wa Kisiwa cha Unguja na Pemba, walifanya kazi kubwa ya kuijenga nchi yao na ndio hadi leo wananchi wanafurahia jitihada hizo hivyo alisema, ni wajibu wa kila mmoja kuziendeleza jitihada hizo kwa faida yao na kizazi kijacho.

## Temeke yakamilisha madarasa 157 ya sekondari

**Na Mwandishi Wetu**

WILAYA ya Temeke mkoani Dar es Salaam imekamilisha ujenzi wa vyumba vya madarasa ya sekondari 157 vilivyogharimu Sh. bilioni 3.14, fedha zilizotolewa na Rais Samia Suluhu Hassan.

Makabidhiano ya vyumba hivyo yamefanyika jana katika Shule ya Sekondari Dovya, Chamazi wilayani Temeke.

Mgeni rasmi katika makabidhiano hayo, Mkuu wa Wilaya hiyo, Jokate Mwegelo, alifafanua kuwa tayari vyumba vyote 157 vya madarasa ya sekondari katika shule 25 vimekamilika vikiwa na meza na viti kwa wanafunzi kukalia.

Jokate alimshukuru Rais Samia kwa kuridhia Wilaya ya Temeke kupewa Sh. bilioni 3.14 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa hayo ikiwa ni sehemu ya fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 kwa wilaya hiyo.

"Tuna deni la kumlipa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuhakikisha watoto wetu wanafanya vizuri katika masomo yao maana fedha alizotupatia ni zaidi ya Sh. bilioni tatu za ujenzi wa madarasa 157, hivyo tutakuwa tumezitendea haki kwa watoto wetu kufaulu," alisema.

**Jokate alimshukuru Rais Samia kwa kuridhia Wilaya ya Temeke kupewa Sh. bilioni 3.14 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa hayo ikiwa ni sehemu ya fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO-19 kwa wilaya hiyo.**




Baadhi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam walivyosherehekea kwa pamoja na Coca-Cola Tanzania katika kuukaribisha Mwaka Mpya wa 2022 mwishoni mwa wiki iliyopita. Kampuni hiyo kupitia kampeni yake inayoendelea ya 'Maajabu Halisi na Coca-Cola' imekuwa ikiendesha matukio tofauti nchi nzima kwa kuwashirikisha watumiaji wa bidhaa zake. PICHA: MPIGAPICHA WETU

## Wanne kortini tuhuma kuiba mali ya msikiti mil. 480/-

**Na Kulwa Mzee**

JAMHURI imemfikisha mahakamani Akshary Motichand na wenzake watatu kwa tuhuma za kula njama na kuiba zaidi ya Sh. milioni 480 mali ya Msikiti wa Shree Sanatan Dharma Sabha.

Washtakiwa walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Godfrey Issaya na kusomewa mashtaka mawili yanayowakabili.

Wakili wa Serikali, Yusuph Abood, aliwataja washtakiwa kuwa ni Motichand (22), Vasant Solanki (73), Ramesh Shah (62) na Shailesh Dhanji (48).

Alidai katika shtaka la kwanza kuwa, washtakiwa wote kwa pamoja kati ya Januari 2016 na Novemba 2016 jijini Dar es Salaam, walikula njama ya kuiba.

Katika shtaka la pili, Akshary anadaiwa katika kipindi hicho jijini Dar es Salaam aliiba Sh. 480,509,088 mali ya Msikiti wa Shree Sanatan, Dharma Sabha.

Washtakiwa walikana kutenda makosa hayo, mahakama ilikubali kuwapa dhamana kwa masharti ya kuwa na wadhamini wawili, wawasilishe fedha taslimu Sh. milioni 60 au hati ya mali isiyohamishika.

Washtakiwa walifanikiwa kupata hati za mali isiyohamishika ambazo zilipelekwa Ardhi kwa ajili ya uhakika kisha zirudi ndipo mahakama itoe dhamana baada ya kujiridhisha.

# Afariki kwa kupondwa na mti akiwa shimoni

**Na Mohab Dominick,** NYANG'HWALE

MKAZI wa Katoro, Julius Ndauli (25), amefariki dunia kwa kupondwa na mti ndani ya shimo alilokuwa akikarabati kuzuia ajali kwa wachimbaji wa madini katika mgodi wa Igalula, wilayani Nyang'hwale, mkoani Geita.

Katika tukio hilo watu watatu wamenusurika kifo na kujeruhiwa sehemu mbalimbali ya miili yao.

Kwa mujibu wa Meneja wa mgodi wa Igalula, Chuma Said, tukio hilo lilitokea Desemba 29, wakati mafundi hao wakiendelea na ukarabati wa shimo (duara) lililohofiwa kuhatarisha maisha ya wachimbaji.

Saidi alidai kuwa zoezi la uokoaji lilianza saa 12 jioni na kufanikiwa kuokoa watu wawili wakiwa hai huku majira ya saa tatu usiku akiokolewa mtu mwingine ambaye alikimbizwa Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale mkoani Geita.

"Kwa mujibu wa sensa ya mafundi waliojiandikisha kuingia katika duara hilo ili kulifanyia ukarabati, ilikuwa ni idadi ya watu wanne na mpaka saa tatu usiku tulikuwa tumeokoa watu watatu, ilibidi tukeshe tunafukua hilo duara mpaka tulipompata Julius Ndauli majira ya saa saba mchana Septemba 30, 2021 akiwa ameshafariki dunia," alisema Chuma.

Aliwataja walionusurika kifo kuwa ni Josephat Andrea, (30), Zabron Mashiri na Charles Masumbuko.

Kutokana na tukio hilo, Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale, Jamhuri William, aliwataka viongozi wa migodi katika wilaya yake kuchukua tahadhari kila wakati ili kuzuia vifo.

Alipofika katika mgodi huo kujionea hali halisi ya mazingira ndani ya eneo hilo, aliwataka wachimbaji kuwa makini huku akitoa wito wawe na desturi ya kuchukua tahadhari kabla ya kuzama maduarani ili kupunguza vifo vinavyotokana na kufukiwa na vifusi vya udongo.

"Ndugu zangu wakazi wa Wilaya ya Nyang'hwale waliofariki dunia ni mtu mmoja tu kati ya watu wanne, na ameshasafirishwa kwenda kwao Katoro kwa ajili ya maziko," alisema Jamhuri.

Kamishna Msaidizi wa Madini Kanda ambaye ni Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Mbogwe, Mhandisi Joseph Kumburu, alibaini ubovu kwa baadhi ya maduara na kuamua kuufunga kwa muda wa siku tano ili yafanyike maboresho zaidi.

"Ndugu zangu wachimbaji nimewaita, tukio hili la mtu kufia duarani chanzo ni wakaguzi wa usalama mgodini kupenda rushwa, hapa wanachukua rushwa kuanzia Sh. 50,000 mpaka 200,000, hivyo nimeufunga mgodi kwa siku tano ili ukarabati ufanyike," alisema Kumburu.



Wakazi wa Wilaya ya Muheza mkoani Tanga wakinunua nguo na vifaa vya shule katika gulio la Jumatatu kwa ajili ya maandalizi ya watoto ambao wanaanza shule mwaka huu, wamedai vifaa vya shule vimepanda bei.
PICHA: STEVEN WILLIAM

# Miaka mitatu gerezani kwa wizi wa pikipiki

**Na Said Hamdani,** LINDI

MKAZI wa Kijiji cha Malungo, wilayani Lindi, Said Nyalle (45), amehukumiwa kifungo cha miaka mitatu gerezani baada ya kupatikana na hatia ya kuiba pikipiki yenye thamani ya Sh. 2,3550,000 mali ya Justine Taabu.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi, Mahakama ya wilaya hiyo, Maria Batraine, baada ya kuridhishwa na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka.

Kabla ya hukumu hiyo, Hakimu Batraine alimuuliza mshtakiwa kama ana sababu zitakazoishawishi mahakama isimpe adhabu kali kwa kesi iliyopo mbele yake, naye aliomba imwonee huruma kwa madai ni mkosaji wa mara ya kwanza na alifanya hivyo kwa njaa.

Baada ya utetezi huo, Hakimu Batraine alimuhoji Mwanasheria wa Serikali, Godfey Mramba kama ana kumbukumbu ya makosa ya zamani kwa mshtakiwa, ambaye aliomba mahakama impe mshtakiwa adhabu kali itakayomwezesha kujifunza na wengine kwamba wizi ni mbaya na haufai mbele ya jamii.

Akitoa hukumu hiyo Hakimu Batraine alisema, hakubaliani na utetezi huo wa njaa alioutoa mshtakiwa na kumhukumu kwenda jela miaka mitatu kujifunza namna ya kufanya kazi halali.

Awali, ilidaiwa mahakamani hapo kuwa Julai 18, 2021 katika Kijiji cha Kingurungundwa, mshtakiwa aliiba pikipiki mali ya Taabu.

# Vodacom yakabidhi zawadi ya gari

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya teknolojia na mawasiliano, Vodacom Tanzania PLC imekabidhi zawadi kwa washindi wa msimu wa furaha inayoitwa "Show Love, Tule Shangwe" pamoja na mshindi mkuu wa kwanza wa shindano la 'Tusua Mapene' aliyejishindia gari jipya.

Akizungumza wakati wa makabidhiano ya gari na zawadi mbalimbali kwa washindi, Mkuu wa mauzo wa Kanda ya Kaskazini, George Venanty, alisema, "Leo hii, tuna mshindi aliyebahatika kujishindia gari jipya kabisa kwa kushiriki katika shindano letu la 'Tusua Mapene'.

"Tumeona itakuwa vizuri ikiwa zawadi hii ya gari ikakabidhiwa wakati tukiwa tunaendeleza msimu wa upendo na kampeni yetu ya "Show Love, Tule Shangwe" kampeni yenye lengo la kurudisha tabasamu kwa wateja wa kampuni hiyo."

Shindano la "Tusua Mapene" liko katika msimu wake wa nne ambapo zawadi zenye thamani ya Sh. bilioni 2.4 ambazo zitatolewa kwa washindi zaidi ya 300,000.

"Tangu msimu wa kwanza wa shindano hili, zaidi ya Sh. bilioni 4.8 zimeshatolewa. Kwa mara ya kwanza magari mapya manne yanakuwa mojawapo ya zawadi zinazoshindaniwa," alisema.

Alisema kampeni ya "Show Love, Tule Shangwe" inalenga kuwapa watumiaji fursa kujishindia zawadi kadha wa kadha, ikiwa ni pamoja na televisheni za kisasa (Smart TV), simu janja na pesa taslimu. Zaidi ya hilo, ili kuendana na msimu wa upendo, zawadi hizi zinagawiwa pia kwa wapendwa ama wenza wa washiriki.

"Katika tukio hili la makabidhiano, televisheni za kisasa 6, simujanja 10 na zawadi za pesa taslimu pia zilikabidhiwa kwa washindi," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kigaigai, Mkuu wa Wilaya ya Moshi Mjini, Abbas Kayanda alisema, Shemmy Malima Chisumo, unavyochukua gari lako, ninakuasa kutumia zawadi hii ambayo ni fursa adimu, kupiga hatua kimaisha na isiwe mwisho wa jitihada zako. Hii iwe hatua ya kwanza kwako, na uendelee kuweka bidii ili upande zaidi kimaisha."

Kwa upande wake, Chisumo aliishukuru kampuni ya Vodacom, na kuwasihi wateja kushiriki shindano la Tusua Mapene, pia wasambaze upendo kwa wapendwa wao ili waweze kujishindia zawadi mbalimbali zinazotolewa katika msimu huu wa sikukuu.

HABARI KITAIFA

# Kafulila aonya makandarasi 'mizigo'

**Na Happy Severine,**
BARIADI

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, ametishia kuvunja mikataba ya makandarasi wa ujenzi wa barabara ambao watatekeleza miradi waliyopewa chini ya kiwango.

Kafulila alitoa kauli hiyo jana wakati wa utiaji saini wa mikataba 19 ya ujenzi wa barabara kwa kiwango cha changarawe na mitaro kati ya Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) pamoja na makandarasi 16.

Alisema makandarasi wote wanaotekeleza miradi ya barabara ndani ya Mkoa wa Simiyu wanatakiwa waondokane na dhana ya kufanya kazi kwa mazoea huku akiwataka wakuu wa wilaya zote kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa mikataba hiyo iliyosainiwa.

"Niwatake makandarasi wote mliopewa zabuni ndani ya mkoa huu, kama kiongozi wa mkoa huu sitosita kuvunja mkataba wa mkandarasi yeyote ambaye nitabaini amejenga chini ya kiwango," alisema Kafulila.

Alisema kuna tabia ya baadhi ya makandarasi wakipewa kazi za ujenzi, wanajenga chini ya kiwango na kumtaja mkandarasi aliyekuwa anajenga barabara ya Matongo.

"Kuna huyo mkandarasi wa Matongo, nataka nipate maelezo kutoka kwa Meneja wa TARURA mkoa, kwanini anaendelea na kazi ndani ya mkoa wakati barabara ile imemshinda licha ya kumtaka arudie, lakini ameshindwa," alihoji.

Katika hatua nyingine Kafulila alisema kwa mara ya kwanza, wananchi wa Mkoa wa Simiyu watashuhudia miradi 18 ya barabara inatekelezwa kwa fedha zao wenyewe ambazo walikatwa kupitia tozo za mafuta.

Awali, akitoa taarifa Kaimu Meneja wa TARURA Mkoa, Mathias Mugorozi, alisema kwa mwaka wa fedha 2021/22 Sh. bilioni 18.2 zitatumika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa barabara.

Alisema kupitia fedha hizo na mikataba iliyosainiwa, kila eneo la Mkoa wa Simiyu kutakuwapo na kazi ya ujenzi na ukarabati wa barabara ili kurahisisha shughuli za maendeleo kwa wananchi.

Pia ujenzi wa miradi hiyo mwisho wa utekelezaji wake ni kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha wa serikali 2012/22, ofisi yake imejipanga kuwasimamia ipasavyo makandarasi wote ili wajenge miradi kwa kiwango kinachotakiwa.

Akizungumza kwa niaba ya makandarasi, Mhandisi Lameck Okech alisema, watahakikisha wanatekeleza miradi waliyopewa kwa kiwango kilicho bora huku akiomba malipo yao yafanyike kwa wakati.

## Ataka vikundi kufundishwa ujasiriamali

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Chalinze, Hassan Mwinyikondo, amemwagiza Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri hiyo kufundisha vikundi vya wajasiriamali mikakati ya kujiinua kiuchumi.

Mwinyikondo alitoa agizo hilo hivi karibuni wakati akizungumza na waandishi wa habari na kusisitiza umuhimu wa vikundi endelevu vitakavyokuwa mfano kwa kufanya maendeleo.

Alisema kuanzishwa kwa majukwaa ya uwezeshaji wanawake kiuchumi ni moja ya sehemu ya kumkomboa mwanamke kutoka kwenye utegemezi na kumwinua na familia anayoiongoza.

"Tumedhamiria wanawake wazidi kwenda mbele hivyo ni vyema wakaelekezwa namna ya kujikwamua kiuchumi waweze kuwa na matokeo chanya kwenye shughuli wanazofanya," alisema.

Alisisitiza vikundi vya wajasiriamali kupewa elimu kabla havijanufaika na mikopo, ili iendane na malengo waliyoyaainisha na kuepuka kuchelewa kurejesha jambo ambalo linawakwamisha wengine kunufaika.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake kiuchumi Halmashauri ya Chalinze, Tatu Bakari, alisema uanzishwaji wa jukwaa hilo ni moja ya sehemu ya kujadili fursa za maendeleo na vikwazo katika shughuli zao.

Aliwaomba wadau mbalimbali kusaidia jukwaa hilo kwa kuwa kwa sasa hawana mapato na pia kupatiwa mafunzo ya uanzishaji wa vyama vya akiba na mikopo.

**Mwinyikondo alitoa agizo hilo hivi karibuni wakati akizungumza na waandishi wa habari na kusisitiza umuhimu wa vikundi endelevu vitakavyokuwa mfano kwa kufanya maendeleo.**



Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, akimfariji mmoja wa majeruhi wa ajali ya gari aina ya Scania Boza aliyelazwa katika hospitali ya wilaya jana. Ajali hiyo ilitokea juzi katika kijiji cha Lidumbe wilayani Newala na kusababisha vifo vya watu 14 na majeruhi 22. **PICHA: ABDALLAH HAMISI**

# RC Njombe awakomesha wanaokwenda mkoani kwake kutafuta 'dada wa kazi'

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Mhandisi Marwa Rubirya, amewakomesha watu wanaokwenda mkoani humo kutafuta watoto wa kuwafanyia kazi za ndani na kwamba serikali itawachukulia hatua kali wazazi/walezi watakaowazuia watoto kwenda kuripoti shule zitakapofunguliwa Januari 17.

Rubirya aliyasema hayo wakati wa makabidhiano ya vyumba vya madarasa 47 vilivyojengwa na fedha za UVIKO-19 wilayani Ludewa.

Alisema mkoa wake hauna watoto wa kuwafanyia watu kazi za ndani, kwa sababu wote wanakwenda shule baada ya madarasa kukamilika kwa wakati ili wakatimize ndoto zao.

Pia, aliwageukia wazazi waliokuwa wakisingizia kukwama kupeleka watoto shule kwa sababu ya michango kwamba kisingizio hicho sasa hakipo.

"Safari hii hakuna kisingizio, huko nyuma mlikuwa mkisema michango mingi, sasa hivi nguvu yote muipeleke kwenye maandalizi ili tunapofungua shule watoto waweze kuanza shule. Sehemu kubwa katika ujenzi wa vyumba vya madarasa Rais ametusaidia kutua mzigo huu, tukalisimamie hilo ndiyo la muhimu zaidi kwa sasa," alisema.

"Kujenga vyumba kama hivi vikakamilika halafu tukifungua shule wanafunzi wasionekane dhamira ya Rais itakuwa haijatimia, kwa hiyo ni kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanaripoti shuleni. Niwaagize mkuu wa wilaya, mkurugenzi, watendaji, madiwani wote katika maeneo yenu kuhakikisha watoto waliochaguliwa na waliopata nafasi ya kujiunga na sekondari tutakapofungua shule waje kusoma," alisema.

Aliwatahadharisha watu wanaoenda mkoani humo kutafuta wafanyakazi wasaidizi wa ndani kuwa mkoa wa Njombe hauna dada wa kazi, unataka watoto wote wakasome ili wafikie ndoto zao na kuwataka viongozi wakalifanyie kazi suala hilo.

Awali, akisoma taarifa ya ujenzi kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Ludewa, Andrea Tsere, Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Sanday Deogratias, alisema ujenzi wa vyumba 47 vya madarasa ya shule za sekondari unakwenda kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

"Hapo mwanzo kabla ya mradi wastani wa wanafunzi 60 walikuwa wanasoma katika chumba kimoja na ifikapo Januari shule hizi zitakua na wastani wanafunzi 40 katika chumba kimoja cha darasa, kwa kufanya hivyo ufanisi utaongezeka katika kujifunza na kupunguza uwezekano wa maambukizi ya UVIKO-19 baina ya wanafunzi na walimu," alisema Deogratias.

# Wasichana 3,000 kujiunga programu elimu ya sekondari kwa njia mbadala

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WASICHANA 3,000 wenye umri kati ya miaka 13 hadi 21 waliokatiza masomo ya elimu ya sekondari kwa walengwa, wanatarajia kuanza masomo yao Januari 17, 2022 katika vituo mbalimbali nchini.

Walengwa hao wanatarajia kunufaika na masomo hayo kupitia mpango wa elimu sekondari kwa njia mbadala chini ya mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari (SEQUIP- AEP).

Lengo la mradi ni kuwapata wasichana 12,000 katika kipindi cha miaka mitano walioshindwa kuendelea na elimu ya sekondari kwa sababu mbalimbali ikiwamo ugonjwa, hali duni ya maisha, kupata ujauzito na kuolewa wakiwa na umri mdogo.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW), Dk. Michael Ng'umbi, alisema mjini hapa wakati akifungua mafunzo ya wadau waliopewa jukumu la kusimamia mradi huo katika uboreshaji wa miundombinu ya madarasa, kujifunzia na kufundishia.

Miundombinu hiyo itatumiwa na walengwa karibu na maeneo walipo ikiwamo vituo vya taasisi hiyo katika mikoa 26 ya Tanzania Bara.

Dk. Ng'umbi alisema wasichana hao ni kati ya 12,000 watakaonufaika na mradi huo wa miaka mitano 2021-2026 wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari nchini.

Aliishukuru serikali kwa kuiwezesha Taasisi hiyo kifedha kwa ajili ya mradi wa kuimarisha ubora wa elimu ya sekondari (SEQUIP- AEP) utakaohusisha ukarabati wa vituo vya uratibu vya mikoa, ujenzi na ukarabati wa vyumba vya kusomea walengwa.

"Tunakusudia hadi kufikia Januari 2022, tuwe tumewasajili wasichana 3,000 ili wawe darasani na uhamasishaji wa kuwabaini na kuwaandikisha umeshaanza kwa kushirikisha maofisa elimu wa wilaya, watendaji kata na vijiji," alisema Dk. Ng'umbi.

Alisema katika utekelezaji wa mradi huo taasisi tayari imeboresha, kuhuisha mitaala na kuandika mipya ya masomo ya Kemia, Fizikia na Stadi za maisha.

Dk. Ng'umbi alisema, mradi huo ni fursa pekee kwa taasisi kuiboresha elimu hiyo ili iweze kuwa shindani na ya mfumo rasmi na kulingana na mwongozo mpya wa elimu kuwa wasichana hao watakaofaulu vyema wataingizwa kwenye elimu ya mfumo rasmi kuendelea na masomo yao ya kidato cha tano.

Kwa upande wake, Mratibu wa Mradi huo kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Baraka Kiomywaki, alisema ni wa miaka mitano unaotekelezwa kwa gharama za Dola za Kimarekani milioni 500 ukiwa ni mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Alisema, awamu ya kwanza ya mwaka mmoja zimetolewa Dola milioni 76 kati ya milioni 500 zilizoingizwa kwenye mkataba kati ya Benki ya Dunia na serikali.

Kaimu Naibu Mkurugenzi, Taaluma, Utafiti na Ushauri wa Taasisi hiyo, Mary Watugulu, alisema hadi Desemba 27, 2021 wasichana wenye sifa zaidi ya 1,500 kati ya 3,000 wamejitokeza kujindikisha katika vituo mbalimbali vya taasisi hiyo nchini kwa ajili ya kujiunga na programu ya elimu ya sekondari kwa njia mbadala.

Watugulu alisema, mikoa inayoongoza walengwa kujitokeza kwa wingi kujiandikisha ni ya Kanda ya Ziwa ya Shinganya na Mwanza na kufuatiwa na Mkoa wa Lindi.




Mkuu wa Idara ya Mtandao wa Wateja wa Benki ya Exim, Agnes Kaganda (katikati), akiongea na waandishi wa habari (hawapo pichani) wakati wa uendeshaji wa droo ya kuwatafuta washindi wa droo ya pili ya kampeni ya 'Weka Mkwanja Tukutoe!' inayolenga kuhamasisha Watanzania kujiwekea amana kupitia benki hiyo iliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Wengine ni ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha, Neema Tatock (kulia) na Meneja Msaidizi wa Bidhaa za Rejareja wa benki hiyo, Callist Butunga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hifadhi Ruhila kutumika kwa sherehe, mikutano

**Na Amon Mtega,** SONGEA

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, amewataka wakazi wa Jimbo la Songea na maeneo mengine kuitumia Hifadhi ya Wanyamapori ya Ruhila (Zoo) kufanyia shughuli za mikutano na sherehe ili kuitangaza hifadhi hiyo.

Dk. Ndumbaro, ambaye ni Mbunge wa Jimbo la Songea, alitoa wito huo jana wakati akizungumza na mamia ya wakazi wa jimbo hilo waliohudhuria sherehe za mwaka mpya wa 2022 katika eneo la hifadhi hiyo ambayo inasimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), ndani ya Manispaa ya Songea.

Akizungumza na wakazi hao, alisema licha ya kuitangaza hifadhi hiyo kwa kwenda kufanyia vikao, wizara pia imejipanga kuboresha zaidi kwa kujenga uzio ambao umeshatengewa fedha Sh. milioni 500 ambazo zimetolewa na Rais Samia Suluhu Hassan kwa lengo la kuboresha sekta ya utalii ili kuwavutia watalii wengi nchini.

Dk. Ndumbaro ameshatembelea milima ya uhifadhi wa Misitu ya Matogoro na kuzungumza na wakazi wa jimbo hilo kuwa katika mikakati ya kuboresha hifadhi hiyo ni pamoja na kuongeza wanyama wakali kama simba, chui, mamba na twiga ili watalii wakifika katika eneo hilo wasikose kuwaona wanyama hao na kuwa amesha-patikana mwekezaji atakayejenga hoteli katika eneo hilo kwa ajili ya wageni wa kutoka mikoa mbalimbali.

Vile vile, alisema akiwa katika hifadhi hiyo alipita kuzungukia baadhi ya maeneo ambayo yemetengwa kwa ajili ya uwekezaji wa vitu mbalimbali akitumia usafiri wa baiskeli.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Songea mjini, Hamis Abdalah Ally, aliwapongeza wafanyakazi wa TAWA kwa kazi kubwa wanayoifanya katika hifadhi hiyo hasa ya kuilinda miti ya asili isivamiwe na watu ambao hawajui maana ya uhifadhi.

Naye Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Ruvuma, Oddo Mwisho, amempongeza Dk. Ndumbaro kwa kutekeleza ilani ya CCM kikamilifu katika sekta ya maliasili na utalii jambo ambalo limesaidia kuwaleta watalii wengi kwenye vivutio mbalimbali nchini.

# Wakulima wahofu uzalishaji wa mazao kushuka

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa mazao ya chakula na biashara Halmashauri ya Ushetu, wilayani Kahama, wametangaza kushuka kwa uzalishaji wa mazao hayo kutokana na mvua chache na kupanda kwa bei za pembejeo.

Kwa muda mrefu wakulima hao wanalima mazao ya chakula na biashara kwa kutegemea mvua, lakini msimu wa kilimo wa mwaka uliopita umekuwa tofauti hali iliyowafanya kuingiwa hofu ya kushindwa kuzalisha zaidi hasa kilimo cha mpunga.

Kadhalika, walidai kupanda kwa bei ya mbolea kutachangia kushusha uzalishaji na kwamba awali walikuwa wakinunua mfuko wa kilo 25 aina ya Kani kwa Sh. 45,000, lakini kwa sasa umepanda hadi kufikia Sh.75,000 hali inayosababisha mkulima mwenye uwezo wa chini kushindwa kumudu gharama.

Waliomba Wizara ya Kilimo kuangalia namna bora ya kushusha bei ya pembejeo ili wakulima walime kwa wingi na kuongeza kipato cha kaya na mapato ya ndani ya halmashauri kwa kuwa inategemea mapato kupitia kilimo.

Walitoa kilio hicho jana wakati wakizungumza na gazeti hili kwa nyakati tofauti, walivyojipanga kukabaliana na changamoto ya uhaba wa mvua na kupanda kwa bei ya mbolea ili kuhakikisha kila mmoja analima mazao yanayostahimili ukame na kujiongezea kipato cha kaya.

Mmoja wa wakulima hao, Bundala Samwel, alisema, kuwapo kwa mvua chache na kupanda kwa bei za pembejeo kutasababisha msimu ujao kupata mavuno kidogo ya chakula na biashara na inaweza ikasababisha Halmashauri ya Ushetu kupata mapato kidogo ikilinganishwa na vipindi vya nyuma.

Naye Magdalena Masanja alisema, mbolea ya kukuzia imepanda kutoka Sh. 60,000 hadi Sh. 105,000 kiwango ambacho ni kikubwa zaidi, na kuiomba Wizara ya Kilimo kuingilia kati kupanda kwa bei hizo ili kuwapatia fursa wakulima kulima kwa wingi.

Diwani wa Kata ya Nyamilangolo, Robert Mihayo, aliwakata wakulima wa halmashauri hiyo kuhakikisha wanalima mazao yanayostahimili ukame ili kukabiliana na baa la njaa hapo baadaye huku akitaja mazao hayo kuwa muhogo, alizeti, mbaazi, viazi na mahindi yanayokomaa kwa muda mfupi.

Hata hivyo, Mihayo aliiomba serikali kuingilia kati na kutatua changamoto ya kupanda kwa bei ya mbolea na kutoa bei elekezi ambayo itakuwa rafiki kwa kila mkulima..

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 4, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 14
**Kampeni ulaji foliki asidi hii hapa**



Ukurasa 12
Mikakati kupaisha ufaulu Mbeya



UVIKO 19 SEKTA YA KAZI
Ukurasa 13
Iharakishe mapitio sheria za ajira, elimu na hamasa kazi zenye staha

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

MTAALAMU:
# Wasichana tunzeni 'vizazi, acheni ngono, dawa kuzuia mimba kiholela

MBOBEZI wa hisabati wa India Anand Kamar, katika moja ya mihadhara yake ya kitaalamu aliwahi kuwaambia wanachuo kuwa elimu ndiyo kiboko pekee cha kuucharaza ujinga na maskini na kufanikisha kujenga jamii yenye usawa. Huo ndiyo ujumbe wa salamu za mwaka 2022 kwa wanafunzi wanaotarajia kuanza masomo Januari 17.

Kalenda inayotumika sasa ni ya mwaka 2022 na ya kale yamekwisha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wakati wanaendelea na likizo yao wanaendelea kutafakari ruhusa iliyotolewa na serikali mwishoni mwa mwaka jana ya kuwaruhusu wasichana wajawazito kurudi nyumbani na kujifungua na baada ya muda wa kulea watoto warudi tena shuleni kumalizia masomo yao.

Ni ruhusa iliyotolewa na serikali, hata hivyo uhuru na fursa hiyo isitumiwe vibaya mabinti wakumbushane kuwa elimu ndicho kiboko pekee cha kuuchapa umaskini na ujinga ambayo ni maadui yanayoshambulia karibu familia zote za Tanzania, hivyo wakiwa waathirika wakubwa wa vishawishi na udanganyifu unaoweza kuwakwamisha kielimu wasione kama kurudi shule baada ya kujifungua ni kufunguka mlango wa mafanikio bali wajikite kusoma na kuachana na dunia hadaa.

Wasichana vyuoni na mabinti wanaosoma shule za msingi na sekondari wajilinde na kuachana na ngono utotoni au kutumia vikinga mimba kienyeji na kuharibu mimba kiholela kwa sababu ni hatari kwao na kizazi kijacho. Ni mambo yanayoweza kuharibu viungo na mfumo wa uzazi.



Mabinti wapewe elimu ya kulinda viungo vya uzazi na kuepusha ngono za utotoni zinazoweza kuhatarisha uzazi. **PICHA: MTANDAO**

Ni ujumbe kwa vijana kwa sababu wengi wao hujihusisha na ngono za utotoni wakitumia mbinu mbalimbali kujikinga na mimba, bila kupata ushauri wa kitabibu, wakifundishana wenyewe kwa wenyewe au kupitia mtandaoni, kwa vile kuna hazina ya elimu, kwenye sekta zote kuanzia afya, elimu, mazingira na malezi, hivyo ikitumika ipasavyo kuna manufaa na kinyume chake ni hasara.

Akizungumzia suala la wasichana na mabinti na ngono pamoja na matumizi holela ya kuzuia ujauzito, bingwa wa magonjwa ya kinamama na uzazi kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dk. Living Colman, anasema kuna matumizi makubwa ya dawa za dharura kuzuia mimba 'P2' kwa vijana hasa mabinti ambao hawajazaa au kuolewa.

"Ukitizama kwenye jamii hasa mijini wengi wanatumia njia ya uzazi wa mpango wa dharura (emergency contraceptive pills au P2) ambayo si sahihi sana, kwani ikitumika mara kwa mara inapoteza maana. Kuwapa watoto dawa za uzazi wa mpango ni kuwaruhusu kufanya ngono ovyo, hali inayosababisha kupata maambukizi kwenye via vya uzazi (PID), kuathiri mirija ya uzazi na kuongeza uwezekano wa kushindwa kupata ujauzito wakati watakapohitaji," anasema bingwa huyo.

Mtaalamu wa magonjwa ya kinamama na uzazi anawataka watoto waache ngono kwa kuwa ni chanzo cha ugumba na maambukizi kwenye via vya uzazi tena katika umri mdogo jambo ambalo ni hatari zaidi.

"Kwanza watoto wafundishwe kuepuka ngono za utotoni, ambazo ndiyo chanzo cha maambukizi PID, kuziba mirija na kushindwa kupata mimba. Mzizi wa ugumba unategemeana na chanzo cha kushindwa kushika mimba, kwa mwanamke chanzo kikuu ni mayai kukosa mpangilio kwenye kupevuka," anasema na kuonya kuwa lakini PID nayo ina mchango mkubwa.

Mwishoni mwa mwaka jana Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), chini ya mwavuli wa Mtandao wa Kusini mwa Afrika (Southern Africa Gender Protocol Alliance), unakutana na asasi za kiraia za 'Women Right Organization' (WRO's) takribani 40, zinazoongozwa na vijana zikijikita katika masuala ya kijinsia ikiwamo afya ya uzazi na ndoa za utotoni.

Yanayojadiliwa ni pamoja na Tanzania kufanya juhudi ndogo, hususan kwenye kutoa elimu ya afya ya uzazi kwa vijana, ambayo ni haki inayotambuliwa na kuelekezwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Kadhalika, Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), linashirikiana na mashirika mengine ya Umoja wa Mataifa na serikali, Azaki, vijana na taasisi nyingine zinazohudumia vijana ili kukuza na kulinda afya ya ujinsia na uzazi na haki za binadamu vijana.

Akizungumza kwenye mkutano huo, unaokutanisha asasi hizo, msimamizi wa idara ya utetezi na ujenzi wa nguvu za pamoja wa TGNP, Joyce Mkina, anasema kuna maeneo ambayo Tanzania haikufanya vizuri ambayo pia yameorodheshwa kwenye Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na kupimwa kupitia 'SADC Gender Protocol.'

INAENDELEA UK.12

ELIMU

NA NEBART
MSOKWA, MBEYA

# Mikakati kupaisha ufaulu Mbeya

- Kuanzisha shule za Kiingereza za umma
- Kuzawadia walimu, wanafunzi wanaong'ara

KUPATA elimu bora ni haki ya kila mtoto na ni moja ya mambo yanayoainishwa kwenye katiba na Sheria ya Mtoto namba 21 ya mwaka 2009, lakini hakuna mafanikio bila mikakati.

Mkoani Mbeya utekelezaji wa mipango mbalimbali ya elimu unaendelea, lakini ukiwa mkoa wenye idadi kubwa ya taasisi za elimu zikiwamo shule za msingi, sekondari, vyuo vikuu na vyuo vya kati, kwa mujibu wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Taarifa hiyo ya mwaka jana, inasema zipo shule za msingi 756 na sekondari 243, ikionyesha kuwa kati ya shule hizo 715 ni za serikali wakati za binafsi ni 41.

Aidha, kati ya sekondari 243 za serikali ni 172 wakati 71 ndizo zinazomilikiwa na wawekezaji binafsi na pia taarifa inaeleza kuwa Mbeya ina vyuo vikuu vitatu, matawi ya vyuo vikuu vingine saba, vyuo vya ualimu sita pamoja na vidogo vidogo 24 vilivyosajiliwa na Mamlaka ya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA).



Naibu Spika Dk. Tulia Ackson. **PICHA: MTANDAO**

### KUONGEZA UFAULU

Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, Majuto Njanga, anasema kwa kushirikiana na wadau mbalimbali mkoa umeandaa mikakati mingi ikiwamo mpango wa kuhimiza kujenga shule za msingi za serikali za mchepuo wa Kiingereza kwa sababu wamebaini mahitaji ya shule hizo ni makubwa.

Anasema kuna mpango wa kutumia njia mbalimbali kuwahamasisha wazazi na walezi kutimiza wajibu wao wa msingi wa kushirikiana na walimu kwenye malezi na kufuatilia maendeleo ya watoto kitaaluma.

Aidha, anataja kujenga shule maalumu ya bweni ya mkoa kwa ajili ya wasichana wanaosoma sayansi wilayani Kyela akieleza kuwa eneo limeshaandaliwa.

Njanga anasema kuhamasisha ujenzi wa sekondari za kata kwenye kata ambazo hazina, aidha shule za msingi kwenye vijiji ambavyo havina ili kuwapunguzia wanafunzi umbali wa kusafiri kwenda shuleni kuwa ni mkakati mwingine unaofuata.

> **"Mwaka 2019 wanafunzi waliofanya mtihani walikuwa 39,420 na waliofaulu walikuwa 34,306 sawa na asilimia 87.03 na mkoa ulipanda kwa nafasi sita na ulishika nafasi ya saba kitaifa.**

### HALI YA UFAULU

Kwa mujibu wa Ofisa Elimu wa Mkoa wa Mbeya, viwango vya ufaulu vya wanafunzi katika ngazi mbalimbali za elimu mkoani humo hasa shule za msingi na sekondari vinapanda na kushuka.

Anafafanua kuwa ufaulu wa mitihani ya kumaliza elimu ya msingi, nao unapanda na kushuka katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2016 mpaka 2020 na kwamba mwaka 2016 wanafunzi waliofanya mitihani ya kumaliza darasa la saba walikuwa 41,972 na waliofaulu walikuwa 25,494 sawa na asilimia 61 na mkoa huo ulishika nafasi 22 kitaifa nafasi ambayo ilikuwa mbaya kuliko miaka yote.

Anasema mwaka 2017 wanafunzi waliofanya mtihani huo walikuwa 45,731 lakini waliofaulu walikuwa 30,916 sawa na asilimia 67.6 na Mbeya ilipanda nafasi tano na kuwa ya 17 kitaifa.

Njanga anasema mwaka 2018 wanafunzi waliofanya mtihani walikuwa 45,469 na waliofaulu walikuwa 34,403 sawa na asilimia 75.7 na mkoa ulipanda nafasi nne na kushika nafasi ya 13 kitaifa.

Anasema mwaka 2019 wanafunzi waliofanya mtihani walikuwa 39,420 na waliofaulu walikuwa 34,306 sawa na asilimia 87.03 na mkoa ulipanda kwa nafasi sita na ulishika nafasi ya saba kitaifa.

### UFAULU SEKONDARI

Njanga anaisifu Mbeya kwa kufanya vizuri zaidi kuliko mitihani ya ngazi zingine kwa maelezo kuwa kuanzia 2016 mpaka 2020 ni mwaka mmoja pekee mkoa huo haukuingia kwenye orodha ya mikoa 10 bora.

Anasema mwaka 2016 waliofanya mitihani walikuwa 23,130 na waliofaulu walikuwa 15,651 sawa na asilimia 67.7 na mkoa huo ulishika nafasi ya 13 kitaifa na kwamba ndiyo mwaka pekee hawakufikia hatua ya 10 bora.

Anasema kuanzia 2017 matokeo yamekuwa bora zaidi na ufaulu umekuwa wajuu kitaifa na kuongeza: "Kwa matokeo ya kidato cha sita mkoa wetu umekuwa ukifanya vizuri sana maana kati ya miaka hiyo mitano ufaulu umekuwa ukianzia asilimia 98 mpaka asilimia 99.33 na kuwa miongoni mwa mikoa iliyokuwa inafanya vizuri zaidi."

### MCHANGO NAIBU SPIKA

Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Akson ambaye ni Naibu Spika, Taasisi yake ya Tulia Trust, ni miongoni mwa wadau wanaochangia kuongeza ufaulu, akiwekeza kwenye madarasa, vyoo na mabweni kwa ajili ya wasichana kwenye shule za msingi na sekondari.

Aidha, mbunge huyo anashirikiana na Ofisi ya Elimu Mkoa kuandaa tuzo za walimu wanaofaulisha, wanafunzi wanaong'ara pamoja na shule zao wote wakipokea zawadi akisema: "Taasisi yangu inaboresha miundombinu kwenye maeneo ya huduma za jamii hasa kwenye afya na elimu kuboresha mazingira ya kusomea watoto wetu hasa wa kike ili tupandishe ufaulu," anasema Dk. Tulia.

### MSISITIZO WA RC

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, anawataka Wakuu wa Wilaya kusimamia sekta ya elimu kuhakikisha ufaulu wa ngazi zote unafikia zaidi ya asilimia 95, na ili kutimiza lengo anahimiza ushirikiano wa walimu, wazazi na serikali na kutaka ila mmoja kutimiza wajibu wake.

Aidha, anaahidi atahakikisha shule zote ndani ya mkoa huo zinakuwa na utaratibu wa wanafunzi kula chakula cha mchana shuleni ili kuongeza ufaulu.

## Wasichana tunzeni 'vizazi, acheni ngono, dawa kuzuia mimba kiholela

INATOKA UK.11

Joyce anasema asilimia 16 ya wanawake wakiwamo wasichana kuanzia umri wa miaka 15 hadi 49, hawajafikiwa na elimu ya uzazi wa mpango, jambo ambalo linasababisha baadhi kutumia vibaya njia za uzazi wa mpango na kuhatarisha kizazi cha sasa na kijacho.

Mshiriki mwingine, akimuunga mkono Joyce anasema: "Ni asilimia 36 pekee ndiyo kiwango cha matumizi ya uzazi wa mpango kati ya wanawake wote nchini, wenye umri wa miaka 15 hadi 49 kwa njia yoyote atakayoichagua mama au msichana. "Kuna matumizi makubwa ya dawa za P2 na ni biashara kubwa kwenye maduka ya dawa za binadamu, ambayo huuza dawa hizi.

"Kuna maduka nilifanya utafiti nikabaini takribani vidonge 2,000,0000 viliuzwa ndani ya muda mfupi katika moja ya maduka yanayouza dawa hizi, wateja wakuu wakiwa wasichana, wanavyuo ambao hawajazaa. Hili lina madhara kwenye uzazi," anasema mmoja wa washiriki jina linahifadhiwa.

### UNFPA YAONYA

Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), linasema kuna mamilioni ya vijana duniani, ambao ujana wao huleta si tu mabadiliko katika miili yao, bali pia udhaifu mpya wa ukiukwaji wa haki za binadamu, hasa katika kujamiiana, ndoa na uzazi.

Linasema mamilioni ya wasichana wanalazimishwa kufanya ngono na kuingizwa katika ndoa zisizotarajiwa, jambo linalowaweka katika hatari ya kupata mimba zisizotarajiwa, utoaji mimba usio salama, magonjwa ya kujamiiana (STIs) ikiwa ni pamoja na Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Aidha, linaongeza kuwa wavulana wamo hatarini na kwamba wanakabiliwa na vikwazo vya habari kuhusu afya ya uzazi na hata ambao wanaweza kupata taarifa sahihi kuhusu afya na haki hiyo, wanakwama kuzifikia huduma hizo.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

UVIKO 19 SEKTA YA KAZI

# Iharakishe mapitio sheria za ajira, elimu na hamasa kazi zenye staha




Madereva wa bodaboda waliohamasika na kujisajili kutetea maslahi yao. **PICHA: MTANDAO**

KARIBU Mwaka Mpya 2022 huenda kuna wanaoutazama kwa matumaini, lakini mioyoni mwa wengine fikra za hofu zimetawala. Swali linalowatatiza linabaki je, UVIKO-19 utaendelea kuvuruga kazi?

Ni kwa sababu COVID-19 imetishia hatima za wengi kiafya na kiuchumi na kukwamisha uwekezaji, biashara, utendaji kazi na kuvuruga ajira.

Ujio wa corona umedhoofisha sekta ya utalii huku baadhi ya wafanyakazi wakikosa stahiki na haki zao kipindi cha UVIKO-19 na baadhi wanaendelea kudai mishahara hata sasa.

Haya yanazungumzwa kwenye mkutano unaoandaliwa na ActionAid Tanzania (AATZ) na wadau wa sekta ya kazi ikiwamo Serikali ya Tanzania na Zanzibar, Azaki, Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (ZANEMA) Chama cha Waajiri (ATE) na wanahabari, kuzungumzia mafanikio ya mradi wa kazi zenye staha unaojikita katika masuala ya waajiriwa kufanyakazi zinazoheshimu haki za wafanyakazi mfano, kupewa mikataba na stahiki zote zinazoelezwa kwenye sheria za ndani, mikataba ya kimataifa, sera na miongozo ya ajira.

Miongoni mwa mambo yanayojadiliwa ni pamoja na Tanzania kufanya juhudi ili sheria na kanuni mahala pakazi zizingatiwe, waajiri watimize wajibu wao na wafanyakazi wapate haki na stahiki kama mshahara kulingana na kazi na taaluma zao, likizo za malipo na za uzazi, bima za matibabu, fidia wakiumia kazini na mafao na pensheni kupitia mifuko ya hifadhi ya jamii.

Katika mkutano huo wadau wa sekta ya kazi wanahimiza kasi ya kurekebisha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya 2004, ili itoe maelekezo ya nini kifanyike wakati majanga yasiyotabiriwa na binadamu kama magonjwa ya mlipuko mfano UVIKO-19, mafuriko au ukame yanapotokea.

Akizungumza katika mkutano huo, wakili Renata Selemani kutoka Taasisi ya Bright Jamii Initiatives ya Dar es Salaam, anasema ni miongoni mwa wadau waliofanya uchambuzi wa sheria mbalimbali kipindi cha UVIKO-19 na kubaini Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, ina upungufu.

"Kuna upungufu mkubwa kwenye sheria hii haisemi hatua za kuchukua wakati yanapotokea majanga yasiyotabiriwa na binadamu, mfano magonjwa kama COVID -19 kulinda stahiki za wafanyakazi ..."

> **Wafanyakazi wa hoteli Visiwani wamekuwa na uthubutu wa kudai haki wakati wa UVIKO-19, badala ya kukubali kurudishwa nyumbani bila kudai stahiki zao.**

Anawaambia washiriki kuwa mapatio ya sheria hiyo na nyingine yaliyofanywa kwa kushirikiana na mashirika ya kutetea haki za wanawake yalibaini kuwa wakati COVID-19 ilipoingia nchini kwa sababu sheria iko kimya waajiri na wafanyakazi kila mmoja alifanya juhudi zake na alikuwa na sababu za kujitetea.

Anasema waajiri walichukua hatua walizodhani zinastahili kwa mfano kuwafungia wafanyakazi ofisini mathalani, wakiingia Jumatatu watatoka Ijumaa.

Renata anasema waajiri wanajitetea kuwa walichukua hatua hiyo ili kuepusha maambukizi waajiriwa wasitoke nje na kukutana na jamii yenye wagonjwa na kuambukizwa na kupeleka maradhi kazini.

Aidha, wapo waliowapa wafanyakazi likizo bila malipo kwa maelezo kuwa kampuni hazina mapato wala njia ya kupata fedha baada ya kukwama kibiashara.

"Kwa mfano, kampuni za kitalii hazikufanya biashara kwa sababu hakuna watalii wanaoingia hivyo, hazikuwa na mapato ya kulipa mishahara. Lakini kuna wafanyakazi waliamua kutokwenda kazini kuhofia kuambukizwa UVIKO -19." Anasema Renata.

Anaeleza kuwa huko ni kuvunja mkataba, lakini yote hayo ni kutokana na ukimya wa sheria haisemi nini cha kufanya wakati wa majanga hayo.

Anasema kinachosubiriwa sasa ni kurekebisha Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, lengo ni kila upande ujue wajibu wake kuanzia, serikali, waajiri na wafanyakazi.

Anakumbusha kuwa watu wengi wa sekta isiyo rasmi waliathirika zaidi, kwani kila mmoja alifanya alichoweza. "Tumewasilisha mapendekezo serikalini yafanyike marekebisho sheria iseme kama kuna majanga yasiyotabirika haki za wafanyakazi zinalindwa vipi na ili kuzuia biashara au uwekezaji usiathirike nini kifanyike," anasema wakili huyo.

ActionAid, inayoshirikiana na wadau kutekeleza mradi wa kazi zenye staha Bara, Zanzibar na Pemba, washiriki wanataja mafanikio yake kuwa ni pamoja na kuwaunganisha wafanyakazi wa sekta binafsi kwenye maeneo mbalimbali mfano uvuvi, bodaboda, hotelini na nyumbani na kuwaelimisha taratibu, sheria, haki wajibu wao na wa waajiri ambao walikuwa hawafahamu kikamilifu.

Kutoka Zanzibar wajumbe wanaeleza mafanikio zaidi kuwa ni kuundwa kikosi kazi kufanya kampeni ya kuhakikisha kunakuwa na kazi za staha Visiwani.

Wajumbe hao wanasema timu hiyo inaundwa na serikali, Jumuiya ya Waajiri Zanzibar (ZANEMA), wafanyakazi kutoka sekta ya umma na binafsi, Chama cha Waajiri, Uhamiaji, Polisi na wanahabari na kwamba ina wajumbe 12.

Wanasema kupitia semina, mafunzo, mikutano na maofisa kazi vijana wanaopata waliohamasishwa wakipata ajira wanakuwa na mwamko wa kudai haki zao kama mishahara, likizo na kupata mikataba ya ajira tofauti na miaka ya nyuma walikuwa kimya.

Aidha, waajiri wameanza kuwapa wafanyakazi mikataba iliyoandikwa kwa Kiswahili tofauti na zamani walipewa iliyokuwa na lugha wasioifahamu, kulazimishwa kusaini tena bila kupewa nakala kama sheria inavyoelekeza.

Aidha, wanasema mradi huo umewafungua waajiriwa akili wamefahamu vyombo vya kutoa haki zao pale zinapovunjwa, hapo nyuma walikuwa hawajui wala kuzifuatilia, wengine waliachishwa kazi kwa hila lakini walikaa kimya.

Wafanyakazi wa hoteli Visiwani wamekuwa na uthubutu wa kudai haki wakati wa UVIKO-19, badala ya kukubali kurudishwa nyumbani bila kudai stahiki zao.

Kwa Bara, mradi wa kazi zenye staha umebadili maisha ya bodaboda ambao wamehamasishwa kuungana kwenye vijiwe, kujisajili, kuwa na utambulisho wa eneo lao na kushirikiana katika changamoto mbalimbali. Kwa mfano maeneo mengi ya Dar es Salaam boda wana umoja, vikundi na utambulisho.

Madereva wa bodaboda zinapoibwa wananyanyaswa na kutuhumiwa kupanga njama na kushiriki wizi na wengine kulazimishwa kuzilipa. Lakini wanapouawa mmiliki wa pikipiki hawajibiki, ni matatizo yanayotajwa.

Aidha, madereva hao wanadaiwa fedha wakati wote na wamiliki bila kujali kuwa wanaweza kuumwa, kufiwa na kuuguliwa.

Mishahara ni changamoto hailingani na kazi anayofanya mwajiriwa, lakini kuna waajiri hawatoi nakala ya mkataba kwa wafanyakazi wao.

ELIMU

**NA SABATO KASIKA**

# Kampeni ulaji foliki asidi hii hapa

- Mabango, vipeperushi kuhamasisha
- Msisitizo lishe bora, uzazi salama




Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Child Help Tanzania, Janet Manoni. **PICHA: SABATO KASIKA**

KAMPENI ya kitaifa ya kutoa elimu ya matumizi ya vitamini inayoitwa foliki asidi imeanza kuwahamasisha jamii kutumia vyakula vyenye vitamini hiyo kupunguza uwezekano wa kupata watoto wenye kichwa kikubwa na mgongo wazi.

Ulemavu huo unaotokana na kukosa lishe bora yenye foliki asidi, kabla na wakati wa ujauzito unaweza kupunguzwa kwa kula vyakula vyenye madini ya chuma kama mboga za kijani, matunda, protini hasa nyama, samaki na mayai ili kuongeza chembe nyekundu za damu mwilini.

Kampeni hiyo inayoanzia Dar es Salaam, inalenga kuhimiza Watanzania kula mlo bora na kwamba wiki ya kwanza ya Januari kila mwaka, inaanza na utoaji elimu hiyo unaoambatana na semina, machapisho na mihadhara ya wadau wa lishe na tiba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Child Help Tanzania, Janet Manoni, akizungumzia kampeni hiyo anasema itawafikia watu kwenye mikusanyiko mikubwa kama vituo vya mabasi na hakutakuwa na mikusanyiko ili kujiepushana UVIKO-19.

"Kutokana na maelekezo ya serikali ya tahadhari ya corona, tutatumia zaidi vyombo vya habari, vipeperushi na mabango. Hali ikitulia tutaendelea na ratiba kama ilivyokusudiwa," anasema Janet.

Watagawa vipeperushi, kuweka mabango ya ujumbe wa lishe bora maeneo mbalimbali na kutumia vyombo vya habari kuwafikia wananchi, anasema.

"Tunaamini kwa njia hiyo, elimu itawafikia wengi wakiwamo wa ndani na nje ya Dar es Salaam katika kipindi hiki cha wiki moja ya kampeni ya uhamasishaji wa kuzingatia lishe bora."

Anasema, Shirikisho la Kimataifa la Kichwa Kikubwa na Mgongo wazi Duniani (International Federation for Spina bifida and Hydrocephalus (IF) limezindua wiki hiyo ya utoaji wa elimu ya matumizi ya vitamini ya foliki asidi.

"Hapa nchini, sisi Child Help Tanzania tunaunga mkono jitihada za shirika hilo, katika kampeni hiyo kwa kutoa elimu kwa umma kupitia majukwaa mbalimbali, vikiwamo vyombo vya habari," anasema.

#### ITAOKOA JAMII

Mratibu wa Mawasiliano wa asasi hiyo, Milton Byemerwa, anasema, kuna umuhimu wadau kuwekeza katika elimu kwa umma kuhusu lishe bora ili kuiokoa jamii na uzazi wa watoto wenye ulemavu.

Anasema, ulemavu huo ni ule utokanao na njia iliyofichika hasa mgongo wazi, na kwamba jamii ikielimika vizuri inaweza kubadilika na kufuata ushauri wa wataalamu kuhusu suala la lishe bora.

> **Hapa nchini, sisi Child Help Tanzania tunaunga mkono jitihada za shirika hilo, katika kampeni hiyo kwa kutoa elimu kwa umma kupitia majukwaa mbalimbali, vikiwamo vyombo vya habari.**

"Elimu hii ya kuzingatia lishe bora ikiwafikia Watanzania, watakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya lishe hasa madhara yatokanayo na lishe duni na njaa iliyofichika," anasema Byemerwa.

Anasema, Asasi ya Child Help Tanzania ina mikakati madhubuti wa utoaji elimu lishe kwa umma lakini mingine inakwamishwa na kuwapo kwa janga la ugonjwa wa corona na hivyo.

"Tulitamani sana kwenda kwenye mikusanyiko ya watu na kuelimisha Watanzania wenzetu. hatua ambayo ninaamini kwamba ingesaidia watu kutuelewa zaidi, lakini inabidi tuzingatie maelekezo ya serikali," anasema.

Anasema, huo ndiyo mkakati wao wa kupunguza udumavu, ulemavu kupitia elimu ya lishe bora inayotolewa na asasi isiyo ya kiserikali ya Child Help Tanzania iliyopo jijini Dar es Salaam.

#### ULAJI UNAOFAA

Upungufu wa virutubishi vya madini chuma na vitamini ya foliki asidi ni miongoni mwa matatizo makuu ya lishe hapa nchini yanayotokana na jamii kutokuzingatia elimu ya ulaji unaofaa.

Miongoni mwa waathirika wakuu wa matatizo hayo ni kinamama watarajiwa na wajawazito, hasa wasipofuata ushauri wa wataalamu wa afya na lishe hivyo kuwaathiri pia watoto wanaozaliwa.

Daktari Bingwa wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu wa Hospitali ya Rufani ya Haydom mkoani Manyara, Dk. Haite Samo, anasema hayo na kufafanua kuwa ulaji wa mlo uliokamilika, wenye kujumuisha vyakula mchanganyiko ni muhimu katika kukidhi mahitaji ya virutubishi vyote vinavyohitajika katika mwili wa binadamu.

Anasema, virutubishi hivyo husaidia katika utengenezaji wa chembechembe nyekundu za damu pia hutengeneza mfumo wa fahamu ikiwamo ubongo na uti wa mgongo. Hivyo upungufu wa vitamini ya foliki asidi kwa wajawazito ni sababu mojawapo ya watoto kuzaliwa na athari mbalimbali katika mfumo wao wa fahamu (Neural Tube Defects (NTDs).

Katika ufafanuzi wake, anasema, hiyo ni pamoja na kuzaliwa wakiwa na uwazi kwenye uti wa mgongo (mgongo wazi), kupasuka kwa midomo (mdomo sungura) na ulemavu wa vichwa vikubwa.

#### JAMII HAIJAFIKIWA

Archard Ngemela, Meneja wa Miradi ya Uongezaji virutubishi kwenye vyakula kutoka Shirikisho la Lishe Duniani (GAIN), anasema, pamoja na kuwapo na sera na sheria mbalimbali za uongezaji virutubishi bado jamii haijafikiwa na elimu.

"Hivyo wiki ya kampeni ya kutoa elimu ya foliki asidi ni muhimu sana sio tu kwa walaji bali pia watunga sera, na kwamba, GAIN na wadau wa lishe duniani wamekuwa na mikakati mbalimbali ya programu za uongezaji virutubishi katika vyakula vinavyotumiwa na watu wengi.

Anavitaja vyakula hivyo kuwa ni vile vinavyosindikwa viwandani kama unga wa mahindi, ngano, mafuta ya kula, chumvi ili kurahisisha upatikanaji wa vitamini muhimu na madini.

"Hata hivyo, pamoja na kuwapo na sera na sheria mbalimbali za uongezaji virutubishi bado jamii haijafikiwa na elimu hiyo hivyo Wiki ya Foliki ni muhimu sana sio tu kwa walaji bali pia watunga sera," anasema.

Anasema, kuna sababu mbalimbali zinazochangia upungufu wa madini chuma na vitamini ya foliki asidi kwa wanawake wajawazito kama vile ulaji duni, kutozingatia ulaji wa vyakula vya asili ya wanyama.

#### NJIA ZOTE ZITUMIKE

Mtaalamu wa lishe kutoka Taasisi ya Chakula na Lishe (TFNC), Walbert Mgeni, anasema, kuna njia na mikakati inayoweza kutumika kukabiliana na upungufu wa madini chuma na vitamini vya foliki asidi kwa wajawazito.

Anataja njia na mikakati hiyo kuwa ni kuzingatia ulaji wa vyakula mchanganyiko, kukazingatia ulaji wa vyakula vyenye madini chuma, vitamini ya foliki asidi na vitamini B12.

"Mfano wa vyakula hivyo ni vya asili ya wanyama; nyama, maini, samaki, dagaa na vingine na vinavyoboresha ufyonzwaji wa madini ya chuma mwilini, mfano vyenye Vitamini C kwa wingi ambavyo ni matunda yenye uchachu kama vile machungwa, limau, ndimu na ukwaju," anasema Mgeni.

Anasema, ni umuhimu wa kuzuia upotevu wa madini chuma mwilini kwa kutumia dawa za kujikinga au kutibu malaria, minyoo na kichocho kama inavyoshauriwa na kutumia chandarua chenye dawa, kusafisha mazingira ya makazi, na kuweka nyavu za madirisha ili kujikinga na mbu wanaoeneza malaria.

"Lakini ni muhimu kuboresha akiba ya madini chuma mwilini kwa kuepuka ujauzito kwa kuzingatia uzazi wa mpango na kutumia vidonge vya nyongeza ya madini chuma na vitamini ya foliki asidi, miezi mitatu kabla ya kushika mimba na wakati wote wa ujauzito, na kuendelea kuvitumia miezi mitatu baada ya kujifungua," anasema.



## HABARI DODOMA

## Aomba tozo za simu ziangaliwe upya kwa wanyonge

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWANGALIZI wa makanisa ya Baptisti Kanda ya Kati, Askofu Antony Mlyashimba, ameishauri serikali kuangalia upya tozo za miamala ya simu ili kutoa ahuweni kwa Watanzania wanyonge.

Mlyashimba, alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali yaliyojitokeza katika kipindi cha mwaka 2021.

Alisema tozo za miamala ya simu zilizopitishwa na Bunge kwa lengo la kuharakisha ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na vituo vya afya ziangaliwe upya.

Alisema, zilipoanzishwa zililalamikiwa na watu wengi nchini kutokana na wakati zilipopitishwa kilikuwa kipindi ambacho uchumi umeporomoka kutokana na janga la UVIKO-19.

"Awali, serikali ilisema tozo zitasaidia kuharakisha ujenzi wa vyumba vya madarasa pamoja na vituo vya afya, lakini wakati ule hatukuwa na mbadala hivi sasa upo mkopo alioukopa Rais Samia wa trilioni 1.3 ambao unafanya kazi hiyo, hivyo basi naiomba serikali iwaondolee tozo wananchi ambayo bado inalalamikiwa kila siku," alisema Mlyashimba.

Katika hatua nyingine, alikemea tabia ya vyombo vya dola kuwanyanyasa viongozi wa dini wanapokuwa wanatumia madhabahu yao kufikisha neno la Mungu katika jamii.

"Vyombo vya dola visiwachagulie cha kuhubiri watumishi wa Mungu kwani wao wapo kwa ajili ya kuponya watu kimwili na kiroho hivyo wanapohubiri hawatumii akili zao bali wanatumia nguvu za Kimungu kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu.

"Watanzania au viongozi wa dini wanapotaka kutoa mambo yao ya moyoni wasizibwe midomo bali wasikilizwe na malalamiko yao yatendewe kazi," alisema. Aliwasihi viongozi wa dini pamoja na serikali nchini kuendelea kudumisha amani na utulivu uliopo kwa kuwa na mwafaka wa pamoja ili kuliunganisha taifa kama ambavyo Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitia.

"Rais mama yetu Samia amekuwa akisisitiza kuwa na mwafaka wa pamoja na kusema kuwa hakuna mwenye hatimiliki ya nchi hii kila mmoja wetu anaowajibu kuhakikisha kuwa amani na utulivu wa nchi hii unaendelea kuenziwa na kulindwa," alisema Mlyashimba.

# Wajasiriamali wa matunda, mboga waonyeshwa fursa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAJASIRIAMALI wanaozalisha matunda na mboga za asili wamehamasishwa kujiunga na mpango wa Slow Food (chakula salama) ili waweze kukuza shughuli zao.

Aidha, kwa kujiunga na mpango huo watapata fursa ya kujifunza uzalishaji wa vyakula hivyo ambavyo kilimo chake hakiharibu mazingira.

Ushauri huo ulitolewa na kiongozi wa Slow Food Africa mtandao wa Tanzania kikundi cha Dodoma, Amandus Chitopela, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Chitopelo alisema mwamko kwa wajasiriamali wa Dodoma kujiunga bado ni mdogo licha ya kuwa kiingilio ni Sh. 25,000 ambayo wajasiriamali wengi wanaimudu. Alisema kikundi kinastahili kuanzia watu watano na kuendelea.

"Kwa Dodoma tuna kikundi kimoja chenye wanachama 16 lengo ni kuhakikisha vyakula vya asili vinaendelea kutumika kama uwele, karanga, mlenda, mboga nyingine za majani za aina mbalimbali na matunda ya asili," alisema.

Pia alisema wanaangalia aina ya mifugo iliyopo ya asili kama ng'ombe, kuku, bata, njiwa na mingineyo.

Alisema kikundi cha Dodoma cha Ndigwa Convivium, kila mwaka kinaandaa mpango kazi kulingana na malengo ya slow food International ikiwamo ya kusimamia miradi midogo ya uzalishaji wa vyakula vya asili.

Alisema ili kuimarisha elimu kuhusu vyakula vya asili na utunzaji wake wanashirikiana na shule zenye bustani kwa kuwapa elimu kwenye filosofia ya slow food.

Alisema elimu hiyo wameipeleka katika shule nyingi ikiwamo ya Marie de Matius ambayo ina bustani ya mboga na matunda.

Alisema wanachama watembelea nchi mbalimbali kujifunza na kuona jinsi gani nchi nyingine zinaendesha kilimo cha mboga na matunda ya asili.

Vuguvugu la slow food duniani lilianzishwa na Carlos Petrini wa Italia mwaka 1989 ili kukabiliana na vyakula vya haraka (fast food) na maisha ya haraka, kusahaulika kwa chakula cha kiasili na watu kutokuwa na haja ya kujua mengi juu ya chakula wanachokula kinatoka wapi, ladha yake na jinsi chaguo la chakula linavyoathiri ulimwengu unaowazunguka.

Mmoja wa wanachama wa Slow Food mkoani hapa, Amina Mpore, alisema imemsaidia kusafiri nchi mbalimbali duniani ikiwamo Italia na Ujerumani ili kujifunza.

Alisema ana bustani ya mboga na matunda ya asili ambayo inampatia lishe bora na hata kuwa na mtandao wa marafiki katika nchi mbalimbali duniani.



Mkuu wa Kitengo cha Kodi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Denis Masani, akifafanua jambo kwa waandishi wa habari (hawapo pichani) walipokutana mwisho wa wiki jijini Dodoma. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

## 'Watanzania chapeni kazi kufikia uchumi wa kati wa juu'

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

ILI Tanzania ifikie uchumi wa kati wa juu, Watanzania wanatakiwa kufanya kazi kwa bidii ikiwamo kutumia fursa mbalimbali zinazo wazunguka ili kujiinua kiuchumi.

Hayo yalisemwa na Katibu Tawala Msaidizi Mkoa wa Dodoma, Aziza Mumba, wakati akifungua semina ya wajasiriamali wadogo wanaojihusisha na uzalishaji wa mvinyo mkoani hapa ilioandaliwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO).

Mumba alisema serikali inaendelea na mnyororo wa thamani hasa katika zao hilo la zabibu na kuwaasa wajasiriamali kutokukata tamaa ili waweze kufikia uchumi wa taifa.

Alisema kwa Dodoma zao la zabibu ni la kimkakati na lengo ni wakulima wauze freshi huku serikali na wawekezaji wakiangalia namna ya kuanzisha viwanda zaidi vya kusindika zabibu ziwe juisi na kwamba tayari kuna viwanda vidogo 18 na vya kati vitatu.

"Nashukuru TBS kwa kufanya haya mafunzo kuwapatia ujuzi na kuwajengea uwezo ili wawe jasiri katika usindikaji wa zabibu jambo ambalo litawasaidia katika kuongeza kipato chao na kupata soko kubwa ndani na nje ya nchi," alisema Mumba.

Alizitaka halmashauri zote Mkoa wa Dodoma kuendelea kutoa ushirikiano kwa TBS wanapoendelea kutoa bidhaa zenye viwango.

Naye Meneja wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) Kanda ya Kati, Nickonia Mwabuka, alisema kuwa TBS imeandaa mafunzo hayo kwa kushirikiana na SIDO lengo likiwa ni kuwajengea uwezo ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ubora na usalama hatimaye kujikwamua kiuchumi.

"TBS inasaidia kupima bidhaa hizi ili ziweze kuwa na soko la kimataifa na mpaka sasa wasindikaji 15 wamefaidikia na mfumo huu na kupitia mafunzo haya yatafanikiwa kwa kiasi kikubwa," alisema Mwabuka.

Kwa upande wao wajasiriamali walioshiriki mafunzo hayo walisema kwamba kwao ni fursa kubwa ambapo wataenda kujifunza namna ya kuboresha bidhaa zao zinazotokana na zabibu jambo ambalo litasaidia kupata masoko na kujulikana ndani na nje ya nchi. Naye Ofisa Kilimo wa Jiji la Dodoma, Agness Woisso, alisema wataalamu wanasema mvinyo mzuri unaanzia shambani hivyo ni lazima wakulima waweze kujua ni namna gani watazalisha zabibu nzuri.

Alisema huko nyuma walikuwa na changamoto ya kutokujua zabibu bora, lakini kwa sasa wanaenda kuwafundisha jinsi bora za kuzalisha.

"Manufaa kwa hapa kwetu mkulima wa kawaida mwenye ekari moja anaweza kupata tani nne mpaka sita tutaendelea kutoa elimu nawashukuru TBS kwani mafunzo haya yanawasaidia kujua ni muda gani wa kupuliza dawa," alisema.





# Askofu Gervas Nyaisonga: Tutaendelea kuonya, kukosoa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

RAIS wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania, Mhashamu Gervas Nyaisonga, amesema kanisa hilo litaendelea kutekeleza wajibu wake wa kuonya, kukosoa na kuelimisha linapoona mambo hayaendi ipasavyo na kamwe lisichukuliwe kama watu wanaohitaji nafasi kwa maslahi binafsi.

Nyaisonga ambaye ni Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki la Mbeya, alitoa kauli hiyo juzi alipozungumza na Nipashe kuhusu msimamo wa kanisa hilo katika kuanza mwaka mpya.

Alisema kanisa hilo lina nafasi ya kuhamasisha watu kufanya mambo kwa utashi na kamwe wasitafsiriwe kwamba wanafanya uchochezi kwa kurejea misingi ya kanisa.

"Nabii anawaelekeza watu yale ambayo ni kweli mbele za Mungu kama kuna jambo linafanyika sio sawa tuna uhakika nalo, tutalisema bila kuogopa, wakati fulani wengine huumia pale linaposikia kanisa limesema jambo, lakini hawajui kwamba nabii ana kazi hiyo kwa kanisa lenyewe au sehemu nyingine wasihisi kama tunatamani madaraka mengine nje ya kanisa bali ni majukumu yetu ya kinabii," alisema Askofu Nyaisonga. Aliwasisitiza waamini kuendelea kuishi katika kweli ya Mungu huku wakihakikisha wanatenda mema na kuhubiri amani ili taifa lisonge mbele kiuchumi na kisiasa.

Alisema jamii inapaswa kuwatambua watumishi wa Mungu kufikisha ujumbe kwa njia mbalimbali, iwe ya sanaa ya maigizo, nyimbo, mahubiri na namna nyingine ambayo ina lengo la kupeleka ujumbe wa kinabii ikiwa ni mchango mkubwa wa kanisa.

Baadhi ya waumini wa kanisa hilo walisema wataendelea kuwa sehemu ya kuhubiri amani kupitia matendo yao katika jamii huku wakiendelea kukemea uovu na maasi pindi yanapotokea.

Katika hatua nyingine, Askofu Nyaisonga alituma salamu za mwaka mpya na kuwataka Watanzania kumshukuru Mungu kwa mapito waliyopitia mwaka uliopita na kuwasisitiza wasikate tamaa waendelee kufanya kazi kwa bidii.

Alisema mwaka 2021 ulikuwa na machungu mengi kwa Watanzania baada ya kuondokewa na viongozi wakuu wa kitaifa akiwamo Hayati Dk. John Magufuli.



Mganga Mkuu wa Hospitali ya Wilaya ya Kyela, Dk. Mariam Ngwere aliyesimama (katikati), akizungumza na baadhi ya wanachama wa kikundi cha IBHASA ambao walitembelea ujenzi wa jengo la wazazi katika hospitali ya wilaya hiyo kuangalia hatua iliyofikiwa juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Hospitali mpya yakabiliwa uhaba wauguzi 260

**Na Grace Mwakalinga,**
BUSOKELO

HOSPITALI mpya ya Halmashauri ya Busokelo, wilayani Rungwe katika Mkoa wa Mbeya, inakabiliwa na uhaba wa watumishi huku wakazi wa eneo hilo wakilazimika kufuata huduma za afya kwenye hospitali binafsi ya Itete iliyopo umbali wa kilometa 20 kutoka makuu ya halmashauri hiyo, Luangwa.

Kwa mujibu wa Kaimu Mganga Mkuu wa hospitali hiyo, Dk. Mayunga Kuyeyema, wanahitaji watumishi 300 na waliopo ni 40 pekee ambao hawatoshelezi mahitaji.

Vile vile, hospitali inakabiliwa na uhaba wa vitanda vya wagonjwa 68.

"Serikali inajitahidi kutuongezea watumishi pamoja na kuboresha miundombinu mingine kama vile vitanda vya kulazia wagonjwa, dawa na vifaa tiba, naamini vikwazo vyote vitashughulikiwa," alisema Dk. Kuyeyema.

Miongoni mwa wakazi wa eneo hilo, Gwamaka Mwakatobe, alisema hospitali hiyo inahitaji miundombinu mbalimbali ili iweze kutoa huduma zake za kitabibu kwa ufanisi.

Asasi ya Rungwe yetu imeiahidi hospitali hiyo kutoa misaada mbalimbali ili kuhakikisha huduma za afya zinatolewa bila vikwazo vyovyote.

# Dk. Tulia akabidhi mil. 470/- ujenzi wa sekondari

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Jimbo la Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson ambaye ni Naibu Spika wa Bunge la Tanzania amekabidhi Sh. milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa sekondari mpya ya Kata ya Itende.

Akikabidhi fedha hizo juzi kwenye mkutano wa hadhara, Dk. Tulia alisema kiu yake ni kuona Jiji la Mbeya linakuwa na shule bora ili kuongeza ufaulu wa wanafunzi pia kusogeza huduma karibu ya wananchi.

Alisema shule hiyo ni utekelezaji wa ahadi aliyoitoa kwa wananchi wa Itende ambao walikuwa wakichangia maendeleo katika shule jirani hivyo ujenzi wa shule hiyo utasaidia kujiletea maendeleo.

"Nawashukuru wananchi kwa kunipa ushirikiano kutekeleza majukumu yangu huku nanyi mkitoa nguvu kazi zenu kwa ajili ya ujenzi wa sekondari hii ya Itende, naamini kikwazo cha watoto kufuata huduma ya elimu mahali pengine kitaisha," alisema Dk. Tulia.

Alisema fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya madarasa manane, vyoo matundu 20, maabara, matangi mawili ya maji yenye ujazo wa lita 20, maabara za sayansi tatu, pamoja na ofisi za walimu.

Dk. Tulia alisema hadi sasa Jiji la Mbeya limepata jumla ya madarasa 92 ujenzi wa vituo vya afya katika kata mbalimbali, miundombinu ya maji na umeme.

Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Amede Ngw'anidako, alimhakikishia Dk. Tulia kuwa taratibu za usajili zinaendelea na wanafunzi wote waliofaulu wataanza masomo Januari, mwaka huu.

Diwani wa Kata ya Itende, Julias Mendagalile, alisema yeyote asiyeshiriki shughuli za maendeleo atachukuliwa hatua za kisheria kama walivyokubaliana.

Livingstone Mwakibinga, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Itende alisema miongoni mwa ahadi alizozitoa wakati wa kampeni ni kuboresha elimu, umeme, miundombinu ya umeme na maji na yote tayari yamefanyika kwa kiasi kikubwa.





# Chaneli ya elimu kutekeleza mtaala kidijitali yazinduliwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar imezindua maudhui ya matangazo ya chaneli ya elimu kwa televisheni na radio ambayo itasaidia kutekeleza mtaala wa elimu kwa ngazi ya maandalizi, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu.

Akizindua Eazy Chaneli katika kituo cha mawasiliano Kwarara nje ya mji wa Zanzibar, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Makazi, Riziki Pembe Juma, alisema chaneli hiyo ni jambo muhimu katika sekta ya elimu kwa njia ya TEHAMA kwa watoto wa Zanzibar hasa ikizingatiwa kuwa dunia ipo katika karne ya sayansi ya teknolojia.

Alisema hatua hiyo pia itasaidia wanafunzi kutumia teknolojia kwa usahihi katika kujifunza na kuleta ubora wa elimu Zanzibar.

"Hatua hii itajenga miundombinu ya kisayansi na kuwajengea uwezo walimu ili nchi kuendana na kasi ya maendeleo," alisema.

Alisema kuwa serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali katika sekta ya teknolojia ikiwamo kujenga mkonga wa taifa ambao umesambazwa nchini kuweka mazingira bora ya uwekezaji na kuimarisha ushirikiano kwa mashirika ya mawasiliano ya intaneti ili kurahisisha upatikanaji wa huduma za kihabari.

Ufunguzi wa chaneli hiyo ni miongoni mwa shamrashamra za miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar, waziri huyo alisema Zanzibar imepiga hatua kubwa za kimaendeleo kwa sababu kabla ya Mapinduzi, kisiwa hicho kilikuwa na shule mbili za maandalizi na sasa zipo zaidi ya 382.

Alisema shule za msingi zilikuwa 62, sasa zipo zaidi ya 381 na kulikuwa na shule nne za sekondari ambazo zimeongezeka na kufikia 734.

Waziri Pembe aliitaka Wizara ya Elimu kuisimamia chaneli hiyo ili iweze kutoa maudhui yanayoendana na nchi na hawatokubali kuona mtu anatumia runinga hiyo kufitinisha jamii kwa matakwa yake binafsi.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis Juma, alisema ni jambo la kupongezwa kuona katika miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar wanaanza kutoa elimu kidijitali ambayo ni hatua kubwa kwa wanafunzi wa Zanzibar na wamejipanga kuongeza mitambo ili kufika mbali.

Aliwataka watendaji wa kituo hicho kuwa wabunifu katika vipindi vitakayoijenga jamii kitaaluma na kufikia malengo ya kituo kutoa elimu.

Kwa upande wake Katibu Mtendaji Tume ya Utangazaji Zanzibar, Suleiman Abdullah, alisema rasilimali ya habari ni muhimu katika kuimarisha umoja na amani na utulivu kwa wananchi wa Zanzibar.

Alisema Tume ya Utangazaji Zanzibar inatoa leseni na chaneli kwa ajili ya kutoa elimu kwa jamii ili kulinda amani, umoja na mshikamano kwa Wazanzibari na kuona wamiliki wa vituo hivyo wanafuata kanuni na silka za utangazaji.

Aliwashauri watendaji wa kituo hicho kusimamia maadili ya utangazaji na wakishindwa hawatasita kuchukua hatua ikiwamo kukifungia kituo.

Alisema katika kuhakikisha suala la utangazaji linasimamiwa ni vizuri kuajiri watangazaji wenye sifa ya habari ili kuona amani, umoja na usalama wa nchi unabaki katika hali nzuri.

Akisoma risala ya kituo hicho, Makame Salim, alisema kituo hicho kina lengo la kuandaa mtaala kwa njia ya kidijitali na masuala ya kijamii ikiwamo elimu, afya na sera ya uchumi wa bluu.



Waziri wa Ardhi na Makazi, Riziki Pembe Juma (kulia), akizungumza na Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis, baada ya uzinduzi wa maudhui ya utangazaji wa chaneli ya Wizara ya Elimu katika kituo cha mawasiliano, Kwarara nje ya mji wa Zanzibar. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## Mrithi wa Maalim Seif kujulikana Januari 29

**Na Mwandishi Wetu**

MRITHI wa marehemu Maalim Seif Sharif Hamad kujulikana Januari 29, mwaka huu, baada ya Chama cha ACT-Wazalendo kufanya uchaguzi wa kuwania nafasi mbalimbali zilizokuwa wazi ikiwamo ya mwenyekiti.

Chama hicho kimetangaza ratiba ya uchukuaji na urejeshaji wa fomu za wagombea wa nafasi zilizokuwa wazi ikiwamo ya uenyekiti wa chama hicho iliyokuwa ikishikiliwa na marehemu Maalim Seif.

Akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi ya chama hicho Vuga, Kaimu Makamu Mwenyekiti Kamati ya Taifa ya Kusimamia Uchaguzi, Fatma Fereji, alisema nafasi zilizokuwa wazi zinazohitaji kujazwa kwa kupigiwa kura ni ya Mwenyekiti wa Chama Taifa, Makamu mwenyekiti upande wa Zanzibar na mjumbe mmoja wa Halmashauri Kuu ya Taifa upande wa Tanzania Bara.

Fatma alisema uchukuaji na urejeshaji wa fomu hizo utaanza leo hadi Januari 17, mwaka huu na Januari 19, Kamati ya uchaguzi ya tume itakaa na kuzihakiki fomu za wagombea, Januari 22 sekretarieti ya kamati kuu itapitia fomu za wagombea.

Alisema Januari 27, Kamati Kuu itapitisha majina kwenda Halmashauri Kuu kwa ajili ya kufanyiwa uteuzi.

"Halmashauri Kuu itafanya kikao chake cha uteuzi wa majina ya wagombea Januari 28 siku hiyo hiyo kutafanyika mdahalo kwa wagombea wa nafasi ya mwenyekiti na makamu mwenyekiti na Januari 29 mkutano mkuu wa taifa utafanya uchaguzi," alisema.

Vile vile, wagombea wote wa nafasi ya uenyekiti na makamu mwenyekiti watachukua fomu katika ofisi ya chama hicho iliyopo Vuga na watazirejesha zikiwa na stakabadhi ya malipo ya Sh. 200,000 inayoonyesha malipo kupitia akaunti ya Chama cha ACT- Wazalendo.

Uchaguzi wa mwenyekiti unatokana na kifo cha aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho Maalim Seif aliyefariki Februari 17, 2021.

# SMZ yadhamiria kuwapa wananchi huduma bora afya

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amesema moja kati ya shabaha ya Serikali ya Zanzibar ni kuwapatia wananchi wake huduma bora za afya na za uhakika.

Hemed alieleza hayo katika ufunguzi wa maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Afya pamoja na jengo la ofisi za watafiti huko Binguni, Wilaya ya Kati, Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema ili lengo hilo kufikiwa hakuna budi kwa watendaji kuhakikisha huduma za uchunguzi wa maradhi katika maabara hiyo zinaboreshwa na kupewa kipaumbele hasa katika kuwajengea uwezo watendaji na kuhakikisha kunakuwapo na vifaa vya kisasa.

Alisema maabara ya kisasa ya utafiti wa afya ni ya kipekee kwa Zanzibar itakayofanya utafiti mbalimbali ikiwamo uchunguzi wa dawa za kitalaamu zinazotumika na zinazotokana na mimea.

"Kutokana na uwapo wa UVIKO-19, maabara hii itatumika kufanya uchunguzi wa ugonjwa huu pamoja na maradhi mengine ya milipuko yanayoathiri jamii," alisema.

Aliwataka watumishi kuzitumia mashine zilizofungwa katika kituo hicho kwa umakini na uangalifu wa hali ya juu ili ziweze kudumu kwa muda mrefu kwa kuwa zimenunuliwa kwa gharama kubwa.

Alipongeza ushirikiano uliokuwapo kati ya taasisi hiyo na nyengine za Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo ya Utafiti na Magonjwa ya Binadamu (NIMR) na Afya ya Ifakara (IHI) na ushirikiano kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Naye Waziri wa Afya Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Ahmed Nassor Mazurui, alisema Serikali ya Zanzibar inaendeleza shabaha yake kwa kuhakikisha vituo mbalimbali vya afya vinaendelea kujengwa ili kuwapatia huduma bora za afya wananchi wake.

Alisema katika ujenzi wa taasisi hiyo ya utafiti wa afya kwa maabara iliyopo Binguni, Sh. milioni 361 zimetolewa na serikali kwa kushirikiana na Swiss Development Corporation ambayo imetoa Sh. milioni 145.

Waziri Mazurui alisema miongoni mwa utafiti uliofanywa ni pamoja na kukamilika kwa nyungu kupitia miti mbalimbali iliyosaidia watu kujifukiza kwa ajili ya kukabiliana na maambukizi ya UVIKO-19.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**MOHAMED ENTERPRISES (T) LTD** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 572 CLM – BOXER.** CHASSIS NAMBA **MD2A21BY2KWH97419.** ENGINE NAMBA **PFZWKH55238.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **WMB/RB/17/2021.**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**NDUGU MOHAMED BAKARI NDEGE** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T877ALZ** aina ya **ISUZU PICK-UP** Rangi Dark Blue yenye Chasis **No. 9864031, Engine No.454597** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba DOD/DOD/RB/611071/2021

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

ATHA AMINIELY SWAI ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI AINA YA TOYOTA BREVIS YENYE NAMBA ZA USAJILI T 481 DNZ KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/RB/TR/ 635/2022

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**YUDA DENIS ATHUMAN** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SCANIA 113M** yenye namba za usajili **T 983 ACB**
Lenye chases namba **1143612**
Injini namba.III8109
Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi
Taarifa ya polisi RB. Namba **IRI/IRI/ RB/607581/2021**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARY HAJI OMARY** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA DYNA** yenye namba za usajili **T 870 DSW** Chassis **No. TRY2200001629,** Engine **No. 1TR0009008.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi. **DOD/DOD/ RB/611381/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya BUKOBA, Kituo cha BUKOBA MJINI Mkoa wa KAGERA.**

**Shauri la Madai Na. 47/2021**
**JINA NA MDAI.......WANGUBO FINANCE CO. LTD**
**JINA LA MDAIWA..........HAPPY ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL-IKO KATOMA-BUKOBA.**

**KUITWA SHAURINI KWA MDENI MHUKUMIWA KWA HAPPY ENGLISH MEDIUM PRIMARY SCHOOL,** Kwamba Mdai ameleta maombi mbele ya Mahakama hii kwa ajili ya utekelezaji wa hukumu ya shauri tajwa hapo juu. Unatakiwa kufika mbele ya Mahakama hii tarehe **13 Mwezi 1 Mwaka 2022.**

**Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama leo tarehe 30 Mwezi 12 Mwaka 2021.**

MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA BUKOBA MJINI

......................................
**HAKIMU**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FIDESI SEVERINI KULAYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA DYNA-PICK UP** yenye namba za usajili **T 219 ARN,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa DOD/DOD/RB/781/2022

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

## Mapacha waliozaliwa kwa siku tofauti washerehekewa

**California,** MAREKANI

MWANAMKE mmoja katika mji wa California, Fatima Madrigal, ameweka historia baada ya kujifungua watoto mapacha, ambao wamepishana dakika 15, mmoja akizaliwa mwaka 2021 na mwingine mapema mwaka mpya 2022.

Fatima na mumewe Robert Trujillo, walipata watoto hao huku mmoja wa kiume akizaliwa Desemba 31 mwaka jana majira ya saa 5:45 usiku aliyepewa jina la Alfredo na baada ya dakika 15 ambayo ilikuwa ni saa 6 usiku wa mwaka mpya 2022, walipata mtoto mwingine wa kike aliyepewa jina la Aylin.

"Kwangu ni ajabu kuwa hawa ni mapacha, lakini si siku wala mwaka mmoja," alisema Fatima katika taarifa iliyotolewa na hospitali alipojifungulia.

Daktari anayefanya kazi katika hospitali hiyo, Ana Abril Arias, aliita hilo ni mojawapo ya tukio la kukumbukwa katika kazi yake.

Pia, vile vile daktari hiyo alisema ni tukio tofauti na nadra, akikumbuka mapacha huko Indiana waliozaliwa kwa siku tofauti, miezi na miongo kadhaa baada ya kuzaliwa kwa dakika 30 tu tofauti, WRTV iliripoti.

Kulingana na ripoti hiyo, mtoto mmoja alizaliwa Desemba 31, mwaka 2019 na mwingine alikaribishwa Januari Mosi, 2020.

**BBC**

## Muungano vyama vya siasa wapinga pendekezo ECOWAS

**Bamako,** MALI

MUUNGANO wa vyama vya kisiasa, umekataa pendekezo la muda wa miaka mitano wa kipindi cha mpito, lililotolewa na Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi (ECOWAS) ambayo inakutana katika kikao maalumu, kuhusu Mali, Januari 9, mwaka huu, mjini Accra

Katika taarifa ya Jumapili, muungano wa "Cadre d'échange", ulisema unapinga kile ilichotaja kwamba ni ratiba ya upande mmoja na isiyofaa ya tarehe ya mwisho ya mpito nchini Mali.

Wanaona kuwa pamoja na kukiuka mkataba, mfumo wake haujajadiliwa na hauwakilishi matarajio ya kina ya watu wa Mali.

Viongozi wa Afrika Magharibi, watakutana katika mkutano wa kilele wa kuhusu Mali Januari 9, mwaka huu, mjini Accra, mwezi mmoja baada ya kuzitaka mamlaka za Mali, kufanya uchaguzi Februari 27, mwaka huu, kama vile utawala wa kijeshi ulivyojitolea kufanya hapo awali na kutishia kuweka vikwazo zaidi mwezi Januari.

Serikali ya Mali, inahalalisha kuongezwa kwa miaka mitano kwa kipindi cha mpito, ikitaja hali ya ukosefu wa usalama, ni tishio tangu wanajihadi mwaka 2012.

**BBC**

# Maandamano yamwondoa Waziri Mkuu Hamdok

**Khartoum,** SUDAN

WAZIRI Mkuu wa Sudan, Abdalla Hamdok, ametangaza kujiuzulu, wiki chache tu baada ya kurejeshwa kwenye nafasi hiyo na uongozi wa jeshi uliochukua madaraka, Oktoba mwaka jana.

Hatua ya Hamdok inakuja kufuatia maandamano ya wiki kadhaa, ambayo yamekuwa yakiendelea jijini Khartoum na miji mingine, kupinga mkataba wa kisiasa uliofikiwa kati yake na jeshi.

Waandamanaji wakiongozwa na vuguvugu la kiraia, wamekuwa wakisema wanataka uongozi wa kiraia na si wa kijeshi chini ya Abdel Fattah al-Burhan.

Kupitia televisheni ya taifa, Hamdok ameelezea sababu za kujiuzulu kwake.

"Nimeamua kutangaza kujizulu, kutoa nafasi kwa mtu mwingine mwanaume au mwanamke kuendelea na kazi katika taifa letu zuri, nimejaribu kwa uwezo wangu wote kuhakikisha kuwa nchi yetu hairudi kwenye mizozo.

"Lakini nchi yetu ilikofika, ipo kwenye hatari kubwa ya kutumbukia kwenye mzozo mkubwa unaitishia uhai wake," alisema Hamdok.

Kabla ya kuchukua hatua hiyo, kulikuwa na maandamano jijini Khartoum, Jumapili na kusababisha makabiliano makali kati ya maofisa wa usalama na polisi, na madaktari wanasema watu wawili wamepoteza maisha na kufikisha idadi ya watu 50 tangu kuanza kwa maandamano hayo mwezi Oktoba mwaka jana.

Kujiuzulu kwa Hamdok, kunaicha Sudan kwenye mzozo mwingine wa kisiasa, katika taifa ambalo limeendelea kuwa na historia ya mapinduzi ya kijeshi.

**RFI**



Abdalla Hamdok, aliyetangaza kujiuzulu nafasi ya uwaziri mkuu, nchini Sudan. **PICHA: MAKTABA**

# Al Shabab yaua sita katika shambulio

**Lamu,** KENYA

TAKRIBANI watu sita wameuawa na vijiji kuchomwa moto na watu wanaoshukiwa kuwa wanamgambo wa Al Shabab katika mji wa pwani wa Lamu.

Polisi wanasema wapiganaji hao waliokuwa na silaha nzito, walishambulia vijiji vya Widho eneo la Majembeni Kaunti ya Lamu, mapema jana.

Gazeti la The Star, limemnukuu Kamishna wa Kaunti ya Lamu, Irungu Macharia aliyethibitisha kisa hicho akisema, operesheni ya kuwasaka wavamizi hao inaendelea.

Hali ya taharuki imetanda katika eneo hilo, huku doria za usalama zikiimarishwa.

Kundi hilo la wanamgambo, limefanya mashambulizi mengi katika kaunti ya Lamu ambayo iko mpakani mwa Somalia katika maeneo yanayofikiliwa kuwa ngome ya kundi hilo, linaloshirikiana na mtandao wa Al Qaeda.

Mwanamume mmoja alikatwa kichwa na wengine watano kupigwa risasi au kuchomwa moto hadi kufa katika shambulizi kwenye kijiji kimoja, kaunti ya Lamu, takriban kilomita 420 Kusini Mashariki mwa mji wa Nairobi, polisi walisema.

Kamshina wa kaunti ya Lamu alidai, washambuliaji wanaoshukiwa ni wanajihadi wa kundi la Al Shabaab lenye uhusiano na kundi la kigaidi la Al Qaeda, lenye makao yake makuu nchini Somalia.

Polisi walisema washambuliaji walimchoma kisu na kumkata kichwa mzee wa eneo hilo na kuichoma nyumba yake, na kumuua mtu mwingine ambaye mwili wake ulipatikana kando ya barabara karibu na hapo.

Maiti za wanaume wengine wanne, zilichomwa moto kiasi cha kutotambulika, zilipatikana katika eneo lingine, kulingana na ripoti ya polisi ambayo shirika la habari la AFP, imeiona.

**BBC/VOA**

# JULIO ACHAMBUA KIWANGO NAMUNGO MAPINDUZI CUP

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Msaidizi wa Namungo FC, Jamhuri Kihwelo 'Julio', amesema uchovu uliotokana na wachezaji wao kucheza mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara ni moja ya sababu ya kutoonyesha kiwango cha juu katika mchezo wa ufunguzi wa Kombe la Mapinduzi dhidi ya Meli 4 City juzi.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar, Namungo iliibuka na ushindi wa mabao 2-1.

**Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kumaliza mchezo huo, Julio alisema licha ya kupata ushindi huo na timu yake kutocheza kwa kiwango kizuri, lakini walijitahidi kupambana kupata alama tatu.**

Alisema wachezaji wao wanastahili pongezi kutokana na uwezo walioonyesha licha ya ratiba ya mechi za Ligi Kuu kubana.

"Timu imecheza vizuri, wachezaji wamejitahidi kwa hali ya juu, licha ya uchovu walionao kutokana na ratiba ya Ligi Kuu pamoja na kusafiri, lakini walionyesha kiwango kulingana na uwezo wao kwa kuwa hawakupata mapumziko baada ya kumaliza michezo ya ligi," alisema.

Aidha, alisema wapinzani wao pia walionyesha ushindani na wamecheza vizuri, lakini bahati haikuwa yao.

Kwa upande wa Kocha wa Timu ya Meli 4 City, Sabri Ramadhani China, alisema licha ya kufungwa, lakini lawama zao wanazielekeza kwa waamuzi kwa kushindwa kuchezesha kwa haki.

"Tumefungwa kihalali tunakubali, lakini waamuzi nao wanaturejesha nyuma yapo mambo ya wazi ambayo tulipaswa kupata sisi, lakini tulinyimwa.

Namumgo itashuka tena dimbani kesho dhidi ya timu Yosso majira ya saa 10:15 alasiri na mchezo wa pili utapigwa saa 2:00 usiku ambapo Azam FC itaumana na Meli 4 City.

**TUMEWASILI...**



Kiungo wa CS Constantine, Msudan Sharaf Eldin Shiboub, ambaye pia aliwahi kuichezea Simba, akiwa na winga raia wa Ivory Coast, Moukoro Cheik Tenena (kulia), ambao watua kufanya majaribio kwa Wekundu wa Msimbazi hao kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi. **PICHA: SIMBA**

## Geita Gold yatesa usajili dirisha dogo

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkabaji mtata wa Geita Gold, Kelvin Nashon (picani chini) Naftali, ameongezewa mkataba wa mwaka mmoja kusalia kuitumikia timu hiyo kwenye michuano mbalimbali.

Kwenye mtandao wake wa instagram, Geita Gold imetoa taarifa rasmi kufikia makubaliano na mchezaji huyo wa zamani wa JKT Tanzania kusaini mkataba mpya, baada ya ule wa mwanzo kuelekea ukingoni mwishoni mwa msimu huu.

Mchezaji huyo alisaini mkataba huo mbele ya Makamu Mwenyekiti wa klabu hiyo, George Mbiligenda.

"Tunayo furaha kuwaarifu kuwa tumefikia makubaliano ya kuingia mkataba mpya wa mwaka mmoja na kiungo wetu, Kelvin Nashon. Awali mkataba wake ulikuwa unamalizika Agosti mwaka huu. Hivyo kwa kusaini mkataba huo mpya, kutamfanya aendelee kusalia ndani ya kikosi cha matajiri wa dhahabu hadi 2023," Geita Gold iliandika katika taarifa yake.

Mbali na kumbakisha kiungo hiyo, Geita Gold ndiyo timu pekee kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara iliyoonekana kulitumia vizuri dirisha dogo la usajili kwa kuongeza wachezaji wengi kuliko timu yoyote.

Mpaka sasa imeshawasajili Adeiyum Selemani na Ditram Nchimbi kutoka Yanga, Aron Kalambo kutoka Prisons, Wilia, Lucian, Juma Nyosso na wengineo.



# Nyota Azam FC avulia kofia kiwango cha Sakho

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO wa Azam FC raia wa Zambia, Paul Katema, ameshindwa kujizuia baada ya kummwagia sifa kiungo mshambuliaji wa Simba, Pape Osmane Sakho, kutokana na kiwango kikubwa alichokionyesha kwenye mechi ya Ligi Kuu wakati timu hizo zilipokutana Jumamosi iliyopita katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Katema amesema Sakho alikuwa kwenye kiwango cha hali ya juu na alistahili kuwa mchezaji bora wa mechi hiyo.

"Hatukuwa makini, tukaruhusu mabao mawili, ni mechi ambayo tulijiandaa kushinda ila bahati haikuwa yetu, nafikiri sasa tutajipanga ili tufanye vizuri. Kwa upande wetu Azam mchezaji aliyecheza vema zaidi ni Frank Domayo kwenye mechi hiyo, lakini kwa Simba yule mchezaji mfupi, Sakho alikuwa vizuri zaidi na alistahili kuwa mchezaji bora wa mechi," alisema Katema.

Mchezaji mwingine wa Azam FC, Ismail Aziz alisema kwenye mechi hiyo, Simba walikuwa vizuri zaidi na wao walikuja na mfumo wa kushambulia kwa kushtukiza na kurudi wote kuzuia.

"Mpira ulikuwa mzuri, tulikuja kutafuta pointi tatu, lakini tumeshindwa kwa sababu Simba walikuwa vizuri sana," alisema.

Kwenye mechi hiyo, Simba ilipata ushindi wa mabao 2-1, na kuendelea kujikita kwenye nafasi ya pili.

Matokeo hayo yanaifanya Simba kuendelea kuifukuza Yanga kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, sasa ikiwa na pointi 24 kwenye nafasi ya pili, pointi tano nyuma ya 'Wanajangwani' hao, lakini Wekundu wa Msimbazi wakiwa na mchezo mmoja mkononi ikicheza mechi 10. Azam iko kwenye nafasi ya saba kwa pointi 15, ikicheza mechi 11.

Ligi hiyo kwa sasa imesimama kupisha michuano ya Kombe la Mapinduzi inayoendelea visiwani Zanzibar, ambapo Simba na Yanga zitaanza kutupa karata zao za kwanza kweye michuano hiyo hapo kesho.

Simba itashuka dimbani dhidi Selem View katika Uwanja wa Amaan saa 10:15 alasiri wakati Yanga ikishuka uwanjani hapo majira saa 2:15 usiku dhidi ya Taifa Jang'ombe.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SPURS WAMTAKA COUTINHO

KLABU ya Tottenham Hotspur inataka kumsajili mchezaji nyota wa Barcelona na Brazili, Philippe Coutinho, 29, kwa uhamisho huru. ***(El Nacional)***

### ALVAREZ SAFI UNITED

MANCHESTER United wako tayari kulipa pauni milioni 16.8 zinazohitajika kwa ajili ya kipengele cha mkataba kitakachowawezesha kumsajili mshambuliaji wa River Plate, Julian Alvarez, 21 Januari. ***(Sport)***

### TRIPPIER ANUKIA NEWCASTLE

NEWCASTLE inakaribia kufikia makubaliano ya kumsajili mlinzi wa kulia wa Atletico Madrid, Kieran Trippier, 31. ***(Athletic)***

### RUDIGER MSHAHARA MKUBWA

CHELSEA watalazimika kutoa ofa ya mshahara mkubwa kwa mlinzi wa kati wa Ujerumani, Antonio Rudiger, 28, ambaye atakuwa akilipwa mshahara mkubwa zaidi kuliko mchezaji yeyote wa 'Blues' hao ili kumshawishi aongeze mkataba mpya. ***(Football Insider)***

### CAVARE KUTUA NORWICH

NORWICH wanaangalia uwezekano wa kuwasajili mlinzi wa kulia, Sion na beki, Guadeloupe Dimitri Cavare, 26, ili kuziba pengo la Max Aarons, ambaye anaendelea kuhusishwa na taarifa za kuondoka katika klabu hiyo ya Carrow Road. ***(Jeunes Footeux via Norfolk Live)***

### ROBERTS AKARIBIA SUNDERLAND

SUNDERLAND inakaribia kukamilisha mkataba na winga wa Manchester City, Patrick Roberts, 24. Raia huyo wa England kwa sasa anacheza kwa mkopo katika klabu ya Ufaransa ya Troyes. ***(Football Insider)***

### ISAK KUTUA ARSENAL

ARSENAL imewatambua nyota wa Real Sociedad na Sweden, Alexander Isak, 22, na nyota wa Lille na Canada, Jonathan David, 21, kama chaguo linalowezekana ili kuimarisha safu yao ya ushambuliaji. ***(The Athletic)***

### RICE AWINDWA UNITED

KLABU ya Manchester United wana matumaini ya kumsajili kiungo wa kati wa Uingereza, Declan Rice, 22, kutoka West Ham ***(Sun)***


### TRAORE AGOMBEWA EPL

KLABU ya Tottenham na West Ham ni miongoni mwa klabu zinazomtaka mshambuliaji wa Hispania, Adama Traore, 25, ambaye Wolves wako tayari kumuuza kwa pauni milioni 20. ***(Telegraph)***

### MBAPPE KWENDA MADRID

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti, amependekeza klabu hiyo ya Hispania itasubiri hadi msimu wa majira ya joto kufanya harakati za kumsajili mshambuliaji wa Paris St-Germain, Kylian Mbappe, 23. Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa, sasa yuko huru kufanya mazungumzo na timu nyingine. ***(Goal)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TUCHEL AMKAANGA ROMELU LUKAKU

## Siwezi kumhakikishia maisha ya kukaa hapa muda mwingi, hili si jambo la kujadiliana...

**LONDON,** England

THOMAS Tuchel amesema hawezi kumhakikishia Romelu Lukaku majaliwa ya baadye ndani ya Chelsea baada ya kumuacha katika mchezo wa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Liverpool, Jumapili.

Lukaku mwishoni mwa wiki hii alinukuliwa na Sky Sport Italia, akisema kwamba hana furaha ndani ya kikosi cha Chelsea na kuwa anaweza kurudi nchini Italia alikokuwa akicheza Inter Milan.

**Tuchel aliamua kumuacha kwenye kikosi chake kwenye mchezo huo wa Ligi Kuu na Jumapili na hivyo kuongeza uvumi wa mchezaji huyo wa Ubelgiji kuondoka pale Stamford Bridge.**

Kocha huyo raia wa Ujerumani aliiambia Sky Sports: "Yeye ni mchezaji wetu. Mara zote kuna namna ya kufanya, lakini siwezi kumhakikisha maisha ya kukaa hapa muda mwingi.

"Hili si jambo la kujadiliana kwa sasa, ngoja tuone siku zijazo."

Tuchel hakufichua kama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ameomba msamaha na amesema hakuna uamuzi wowote ambao umefanywa kuhusu kusalia katika klabu hiyo.

Chelsea wako nyuma ya vinara Manchester City kwa pointi 10, huku Liverpool wakiwa nyuma kwa pointi moja, lakini wakiwa na mchezo mkononi.

CHEZA USHINDE KASINO

MECHI KALI

HOME ULINZI STARS 2.85 | 2.80 | 2.56 KARIOBANGI SHARKS AWAY

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa, vodacom m-pesa, halopesa, airtel money, zantel EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# XAVI KUMBAKIZA DE JONG



**BARCELONA,** Hispania

XAVI amependekeza kuwa Luuk de Jong anaweza kubaki Barcelona baada ya dirisha dogo la usajili la Januari.

Mkopo wa De Jong kutoka Sevilla ulitarajiwa kusitishwa mwezi huu kabla ya mshambuliaji huyo kujiunga na Cadiz ya LaLiga kwa muda uliosalia wa msimu huu.

Lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi alihitajika dhidi ya Mallorca wakati Barca itarejea uwanjani Jumapili kutokana na msururu wa kesi za COVID-19 katika kambi ya 'Blaugrana' hao.

Baada ya kugonga mwamba mara mbili, De Jong alifunga bao lake la pili la ligi kwa kichwa dakika ya 44 na kuwapatia Barca ushindi wa 1-0 mjini Palma. Kwa kufanya hivyo, akawa mchezaji wa kwanza wa Barca zaidi ya Lionel Messi kufunga goli mara mbili katika mchezo mmoja wa LaLiga tangu Agosti 2019.

Na huku Xavi akiwa bado anasubiri wachezaji wengine kurejea katika utimamu wa mwili, alidokeza kwamba De Jong bado anaweza kubaki Camp Nou kwa kipindi kilichosalia cha 2021-22.

"Yeye ni mfano," alisema Xavi katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi. "Inasemekana anaweza kutoka, lakini anafanya kazi, anajitoa mhanga.

"Nimefurahishwa naye, bila shaka namwazia kubaki kwa sababu leo (juzi) amekuwa na manufaa kwetu, ni mfano kwa kila mtu. "Kulingana na jinsi unavyofanya mazoezi, utacheza. Tutaona siku zijazo. Tutaona kama kuna njia za kutoka na za kuingilia. Lakini zote ni dhana."



# *Mazungumzo mapya kuirejesha Super League*

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid, Barcelona na Juventus wameripotiwa kufanya mazungumzo mapya kuhusu kufufua European Super League, ikiwa ni miezi minane tangia pendekezo hilo kuzinduliwa.

Mradi huo ulitangazwa kwa mara ya kwanza Aprili 2021 na ulijumuisha makubaliano ya klabu ya Manchester United, Manchester City, Liverpool, Chelsea, Arsenal, Tottenham Hotspur, AC Milan, Inter Milan na Atletico Madrid.

Wazo hilo lilisababisha utata katika Jumuiya ya Soka Ulaya na klabu nyingine vikajiondoa, lakini Real Madrid, Barcelona na Juventus wote walishikilia msimamo wa wazo la kuanzisha European Super League.

Kwa mujibu wa The Mirror, maofisa wakuu kutoka kwa klabu tatu zinaz[illegible] ka wote wamekuta[illegible] wako tayari kuzindu[illegible] pendekezo lao la [illegible] League.

Florentino Perez, [illegible] Laporta na Andrea A[illegible] wanasemekana kul[illegible] ana, mnamo Oktob[illegible] ya mabadiliko m[illegible] muhimu ya kanu[illegible] mashindano yaliyop[illegible] kezwa katika jaribio [illegible] kwanza la kufufua [illegible] League.

## HABARI MICHEZO

# AZAM FC YAZITAKA TATU ZA MELI 4 CITY

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MENEJA Msaidizi wa Azam FC, Rashid Said, amesema kikosi cha timu hiyo kipo vizuri na kimejiandaa kupambana kutafuta alama tatu katika mchezo wao wa leo dhidi ya Meli 4 City kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi.

Azam itashuka katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 2:15 usiku wakiwakaribisha Meli 4 City ambao wametoka kupoteza mchezo wao wa kwanza dhidi ya Namungo.

Akizungumza na waandishi wa habari kuelekea mchezo huo, alisema kwa ujumla kikosi chake kimejiandaa kushinda na wamekuja na wachezaji wao wote. Alisema wachezaji wao wote ambao wamesajiliwa katika msimu huu, watacheza michuano hiyo ya Mapinduzi na kwa wale ambao wana majeraha yaliyotokana na Ligi Kuu Tanzania Bara pia wapo Zanzibar wakiendelea na mazoezi mepesi.

Alisema timu hiyo imejipanga kufanya vizuri katika michuano ya mwaka huu, hivyo wamekiandaa kikosi chao kuhakikisha kinacheza kwa malengo.

"Tumekuja na kikosi chetu chote, kwakuwa tutakuwa hapa Zanzibar kwa muda, hivyo tumeamua kuja na wachezaji wetu ambao ni wagonjwa kwa sababu wataendelea na mazoezi kidogo kidogo na wenzao ambao watakuwa wanacheza michezo ya kombe hili," alisema.



Kiungo wa Azam FC, Ibrahim Ajib, akiwa mazoezini na timu yake visiwani Unguja jana kujiandaa na mechi ya Kombe la Mapinduzi leo dhidi ya Meli 4 City. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Lema kuisuka tena Yanga Princess*




**Na Saada Akida**

LICHA ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya JKT Queens juzi, Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, amesema bado ana kazi kubwa ya kufanya katika kuhakikisha anakijenga kikosi chake kuwa imara zaidi kuelekea michezo yao ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara inayoendelea.

Hata hivyo, wakati Lema akiyasema hayo, Kocha Mkuu wa JKT Queens, Azisho Kondo, alisema kukosekana kwa baadhi ya nyota wao kumeifanya timu hiyo kutofanya vizuri.

Makocha hao walitoa kauli hizo wakati wakizungumza na Nipashe baada ya dakika 90 kukamilika katika mchezo wa ligi hiyo uliopigwa Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Lema alisema licha ya kupata ushindi, mechi hiyo ilikuwa ngumu na ushindani mkubwa, lakini anataka kuhakikisha kikosi chake kinakuwa makini zaidi wakati huu wakielekea kujiandaa na michezo iliyopo mbele yao.

Alisema kulingana na mechi tatu walizocheza ameona ugumu na ushindani uliopo katika ligi hiyo, hivyo anataka kuhakikisha wanakuwa makini zaidi.

"Ligi msimu huu imekuwa na ushindani mkubwa, ukiangalia timu nyingi zimefanya usajili mzuri, kwa upande wetu licha ya kupata pointi tatu, lakini tumefanya makosa mengi, hivyo tunapaswa kuyafanyia kazi kabla ya mechi ijayo," alisema Lema.


LIVE IN PLAY

SPORTPESA APP

BET LEO UWE MILIONEA




MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 04 - JANUARI 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 2032 | Tooro United vs Express FC | 10.60 | 4.82 | 1.25 |
| 15:00 | 2182 | Ulinzi Stars vs Kariobangi Sharks | 2.85 | 2.80 | 2.56 |
| 15:00 | 3609 | Kenya Police vs Vihiga Bullets FC | 1.67 | 3.31 | 5.00 |
| 15:00 | 3842 | Mathare United vs Kenya Commercial Bank | 5.59 | 3.37 | 1.60 |
| 15:00 | 4413 | Sofapaka vs Bandari | 2.99 | 2.85 | 2.41 |
| 15:00 | 4960 | Wakiso Giants FC vs Bul FC | 2.55 | 3.08 | 2.60 |
| 15:00 | 5041 | Gaddafi FC vs Uganda Revenue Authority FC | 6.20 | 3.65 | 1.60 |
| 15:00 | 5295 | Bright Stars vs SC Villa | 2.75 | 2.90 | 2.56 |
| 15:00 | 5398 | FC Saints vs Police FC (UGA) | 1.93 | 3.23 | 3.67 |
| 15:00 | 5633 | Dove All Stars vs Vipers SC | 7.60 | 4.40 | 1.43 |
| 15:20 | 5892 | Alshoulla vs AL Akhdood | 1.54 | 3.66 | 5.59 |
| 15:30 | 4903 | AL Khlood vs AL Nahdha | 2.61 | 2.94 | 2.65 |
| 15:40 | 2704 | Najran SC vs Al Qadisiyah | 3.61 | 3.08 | 2.00 |
| 16:00 | 2913 | SC Ain Defla vs MC Saida | 4.13 | 3.17 | 1.84 |
| 16:00 | 4241 | USM EL Harrach vs Ben Aknoun | 2.24 | 3.03 | 3.08 |
| 16:00 | 4400 | CA Batna vs Ain M'lila | 1.98 | 2.98 | 3.85 |
| 16:00 | 4717 | MO Bejaia vs IRB Lakhdaria | 1.71 | 3.08 | 5.20 |
| 16:00 | 4947 | ASM Oran vs CRB Ain Ouessara | 1.67 | 3.31 | 5.00 |
| 16:00 | 4988 | MO Constantine vs JSM Bejaia | 2.47 | 2.95 | 2.81 |
| 16:00 | 5358 | Hamra Annaba vs MC EL Eulma | 1.53 | 3.51 | 6.16 |
| 16:00 | 5463 | JSM Skikda vs USM Annaba | 2.43 | 2.90 | 3.30 |
| 16:00 | 5760 | WA Boufarik vs ZR Temouchent | 2.99 | 2.29 | 3.04 |
| 16:00 | 5775 | US Chaouia vs Irb Ouargla | 1.57 | 3.52 | 5.59 |
| 16:10 | 3610 | Lekhwiya SC vs Al Khoor | 1.06 | 9.08 | 20.30 |
| 17:00 | 3668 | Bengaluru FC vs East Bengal | 1.59 | 4.05 | 4.44 |
| 17:35 | 5924 | Kazma SC vs AL Qadsia | 2.60 | 3.23 | 2.46 |
| 17:45 | 3271 | Cordoba B vs AD Ceuta B | 1.41 | 4.13 | 6.72 |
| 17:45 | 5939 | AL Khalidiyah vs Al Hala Muharraq | 1.76 | 3.27 | 4.42 |
| 18:00 | 3508 | Lealtad vs Urraca CF | 2.08 | 2.94 | 3.57 |
| 18:15 | 3283 | PAS Giannina vs Ionikos Nikea FC | 1.72 | 3.45 | 4.93 |
| 18:20 | 2625 | Al Rayyan SC vs Umm-Salal SC | 1.69 | 3.75 | 4.13 |
| 18:20 | 5817 | Al Arabi Doha SC vs AL Wakrah | 1.41 | 4.24 | 6.55 |
| 18:30 | 5172 | Jeddah Club vs Hajer Club | 1.59 | 3.68 | 5.04 |
| 19:00 | 3159 | Tenisca vs CD Tenerife B | 2.69 | 2.98 | 2.55 |
| 20:20 | 3714 | East Riffa vs Najma Manama | 1.73 | 3.42 | 4.33 |
| 20:30 | 2187 | Asteras Tripolis vs OFI Crete | 1.97 | 3.11 | 4.05 |
| 22:00 | 2245 | Charlton vs MK Dons | 2.19 | 3.31 | 2.93 |
| 22:00 | 2343 | Oldham vs Wigan | 4.62 | 3.94 | 1.59 |
| 22:00 | 4549 | Crewe vs Rotherham | 4.73 | 3.96 | 1.57 |
| 22:00 | 5095 | Harrogate vs Carlisle | 1.76 | 3.57 | 3.95 |
| 22:00 | 5247 | Hartlepool vs Bolton | 2.80 | 3.28 | 2.28 |
| 22:30 | 2347 | Wimborne Town vs Truro City | 3.56 | 3.75 | 1.81 |
| 22:30 | 5959 | Orihuela CF vs FC J. Espanol de San Vicente | 1.68 | 3.27 | 5.00 |
| 22:45 | 1159 | Alvechurch vs Coalville Town | 3.00 | 3.80 | 2.17 |
| 22:45 | 1168 | Nuneaton vs St Ives Town | 1.95 | 3.95 | 2.98 |
| 22:45 | 2092 | Sutton United vs Colchester | 1.81 | 3.41 | 3.94 |
| 22:45 | 3319 | Cliftonville Belfast vs Crusaders Belfast | 2.79 | 3.42 | 2.22 |
| 22:45 | 5733 | Forest Green vs Exeter | 1.73 | 3.72 | 4.31 |
| 23:00 | 1118 | Lens vs Lille | 2.32 | 3.26 | 2.96 |
| 23:00 | 3921 | Ponferradina vs Espanyol | 3.05 | 3.20 | 2.30 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumanne Januari 4, 2022
Nipashe



Tuchel amkaanga Lukaku UKURASA 21

# Pablo sasa alitaka Kombe la Mapinduzi

## Asema malengo ni kuanza mwaka na ubingwa huku akilenga michuano ya...

**Na Saada Akida**

HUKU akitua visiwani Zanzibar akiwa na kikosi chake kamili bila kuacha hata mchezaji mmoja, Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, ameweka wazi kuwa hataki kuacha kitu msimu huu ikiwa ni pamoja na kubeba Kombe la Mapinduzi kwenye michuano hiyo inayoendelea visiwani humo.

**Simba ambayo iliwasili visiwani Zanzibar jana, kesho itashuka dimbani kutupa karata yake ya kwanza kwenye michuano hiyo kwa kucheza dhidi ya Selem View mchezo utakaopigwa Uwanja wa Amaan majira ya saa 10:15 alasiri.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Pablo alisema wamekwenda kwa ajili ya kushinda pia kuhakikisha wanarejea Dar es Salaam na kombe hilo ambalo litakuwa la kwanza kwa Simba mwaka 2022.

Alisema licha ya uwapo wa wachezaji wake wote, atafanya mabadiliko ya mara kwa mara ya kikosi ili kuwalinda wachezaji kwa sababu wana majukumu makubwa baada ya mashindano hayo.

"Malengo yetu ni kuhakikisha tunatoa ushindani na kutwaa ubingwa, hatukufanya vizuri kwa zaidi ya miaka mitano iliyopita na tunataka kubadili upepo na kuwa mabingwa wa michuano hii," alisema Pablo.

Alisema wanahitaji kufanya vizuri pamoja na kuyatumia mashindano hayo kama mazoezi kwa kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika mechi zilizopita ili kujiweka tayari kuelekea michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika na Ligi Kuu itakaporejea.

"Hii michuano ni muhimu sana kwetu, tukiwa na malengo ya kutwaa ubingwa pia kuimarisha kikosi chetu kuelekea katika michuano mingine iliyopo mbele yetu," alisema kocha huyo.

Ubingwa wa michuano hiyo unashikiliwa na Yanga, ambayo iliutwaa mwaka jana kwa kuwafunga watani zao wa jadi, Simba kwenye Uwanja wa Amaan Zanzibar kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya kutoka suluhu kwa dakika 90 za mchezo.

Kuhusu usajili, Pablo alisema tayari amewakabidhi ripoti viongozi na anahitaji wachezaji watano ambao watasaidia timu hiyo katika kufikia malengo yao waliyojiwekea.

"Nafasi za awali ni beki na viungo ambao watakuja kuleta ushindani mkubwa kwa wachezaji waliopo na kusaidia timu kufikia malengo yetu," alisema kocha huyo.

Wakati huo huo, uongozi wa Simba umemtambulisha, Ahmed Ally, kuwa ofisa habari na mawasiliano wa klabu hiyo kuchukua nafasi ya Haji Manara ambaye alitemana na klabu hiyo.

Simba ipo nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa pointi tano nyuma ya Yanga iliyopo kileleni na alama zake 29 baada ya kushuka dimbani mara 11 huku Wekundu wa Msimbazi hao wakiwa mchezo mmoja nyuma.

MTAJUA HAMJUI!...



Ndiyo hivyo tena! Imeelezwa kilichobaki ni muda tu kabla kiungo wa zamani wa Simba, Clatous Chama kutangazwa kurejea tena kuitumikia klabu hiyo. **PICHA: MTANDAO**

## Kaze apewa majukumu Yanga Z'bar

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha wachezaji wa Yanga kinatarajiwa kuondoka leo mchana kuelekea mjini Zanzibar kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi ambayo tayari imeshaanza kutimua vumbi katika Uwanja wa Amaan.

Ofisa Habari wa klabu hiyo, Hassan Bumbuli, ameliambia Nipashe kuwa kikosi chote cha wachezaji wa klabu hiyo kitakwenda huko na kitakuwa chini ya Kocha Msaidizi, Cedric Kaze.

"Kikosi kitaondoka kesho (leo) kwenda Zanzibar, ambaye hatokuwapo ni Kocha Mkuu Nasreddine Nabi kutokana na kuwa na udhuru, lakini Kaze yeye atakuwapo kusimamia timu, kwa hiyo wanachama na mashabiki wa Yanga mjini Zanzibar wasiwe na wasiwasi kwani wachezaji wote watawaona," alisema Bumbuli.

Yanga imesema kuwa imepania kulichukua tena kombe hilo kwa mara nyingi tena, hivyo hawatokuwa na dharau yoyote kwenye michuano hiyo.

Mwaka jana, Yanga ilitwaa kombe hilo kwa kuwafunga watani zao wa jadi Simba kwenye Uwanja wa Amaan Zanzibar kwa mikwaju ya penalti 4-3, baada ya kutoka suluhu kwa dakika 90 za mchezo.

Yanga itaanza kampeni yake ya kulitetea kombe hilo Jumatano usiku majira ya saa 2:15 usiku itakapocheza dhidi ya Taifa Jang'ombe kwenye Uwanja wa Amaan.

Ni mechi ambayo itatanguliwa na watani zao wa jadi, Simba ambao watacheza siku hiyo hiyo saa 10:15 alasiri kwenye uwanja huo huo dhidi ya Selem View.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >